Jumapili Machi 17, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581618

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Malalamiko** 13,500 wananchi Sema na Rais yapokewa rasmi UK. 2

**Mfanyakazi** wa kampuni ujenzi afia gesti akiwa na mpenzi wake UKURASA 3

**KUELEKEA MIAKA 3**



Samia na dhamira ya kuondoa giza mijini na vijijini UKURASA 8



**PICHICHI TURBAN: 'MBUNIFU ANAYETHAMINIWA TANZANIA'** UKURASA 13



## RIPOTI MAALUMU

# Simulizi 'mchongo' mabinti wa kazi wanaopokewa mijini

• **Wakimbia** kuozeshwa, waangukia ukatili wa mabosi... *Uk. 4*

UKURASA WA 17

## TAASISI KIMBILIO MIKOPO NAFUU KWA WAJASIRIAMALI



Mfuko wa SELF umekuwa mkombozi na kimbilio la wajasiriamali wadogo na wakati kwa kuwakopesha mabilioni ya shilingi na matunda yake yameonekana...

# Sumu ya nyuki kutibu maradhi saratani, Ukimwi

UKURASA 2




Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akikabidhiwa tuzo na Waziri wa Mapato wa Jamhuri ya Ethiopia, Aynalem Nigusie (kulia) na Mwenyekiti wa Jarida la Uongozi Afrika, Dk. Ken Giami, kwenye hafla ya kila mwaka ya Tuzo za Watu Bora wa Mwaka za ALM, Addis Ababa, Ethiopia, jana. **PICHA: OFISI YA RAIS MSTAAFU**

## AGNETHA BAHIGWE

UKURASA 3

# Binti wa miaka 24, 'jembe' la kutegemewa mochwari

**MICHEZO** NI MECHI YA KISASI, UBABE UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Mgonjwa kuchagua daktari Muhimbili

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH) imetangaza huduma mpya ambayo mgonjwa atakuwa na uwezo wa kumchagua daktari amtakaye kwa kujisajili kwa njia ya mtandao na kupanga naye muda wa matibabu.

Ofisa wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Hospitali ya Muhimbili, Chindemba Lingwana, alisema huduma hiyo ni katika kuendana na kasi ya sayansi na teknolojia.

"Mfumo huu utamwezesha mgonjwa kufanya usajili na kumchagua daktari anayemtaka, kliniki anayotoka, huduma anayoitaka na kwa muda anaoutaka. Mfumo ni rahisi na ni rafiki kuutumia unaweza kuomba ukiwa hata nyumbani.

"Hii inasaidia kumpunguzia mgonjwa usumbufu wa kuja kusimama hospitalini. Mfumo huu ni salama na wa siri kumbukumbu zote za mgonjwa zinatunzwa kwa usalama, hataweza kuuona mtu mwingine," alisema Lingwana.

Alisema ili mtu kupata huduma hiyo anatakiwa kutumia simu au kompyuta mpakato (laptop) na kufungua kivinjari (browser) na kuingia kwenye tovuti ya Hospitali ya Muhimbili. "Ukiingia hapo kulia utaona Appointment utabonyeza itafunguka na njia ya pili ukiwa umefungua browser yako utaandika www.appointment.mnh.or.tz mfumo utafunguka na utaanza kujaza taarifa zako kwa kuandika jina lako la kwanza na la pili.

"Utaandika namba ya simu, utajaza email yako na kuchagua kliniki unayokwenda na kumchagua daktari na muda unaotaka kuonana naye kisha kutatuma," alisema Lingwana.

Alisema baada ya hatua hizo mhusika (mgonjwa) atapokea ujumbe katika simu yake au kwenye email yake kumtaarifu kuwa taarifa zake zimepokewa.



Msimamizi wa Uchaguzi wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zaituni Said akitoa maelekezo wakati wa semina ya mafunzo ya siku moja kwa Makalani waongozaji wapigakura uchaguzi mdogo wa udiwani kata ya Mkuzi, yaliofunguliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Dk. Jumaa Mhina (hayupo pichani), jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Sumu ya nyuki kutibu saratani, UKIMWI

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amesema utafiti unaendelea kufanywa na wataalam kuhusu sumu ya nyuki ambayo inauzwa kwa Sh. milioni 150 kwa kilo na kuna matumaini huenda itatumika kutibu maradhi sugu kama saratani na UKIMWI.

Akifungua Mkutano Mkuu wa Wafugaji Nyuki wa Mkoa wa Singida ulioandaliwa na Kampuni ya Kijiji cha Nyuki, Pinda alisema chanzo cha sumu ya nyuki kuuzwa ghali ni kutokana na utafiti unaoendelea.

Katika mkutano huo pamoja na mambo mengine, wafugaji walipitisha rasimu ya mwisho ya kuundwa kwa umoja wa wadau wa nyuki Mkoa wa Singida na kugawiwa mizinga 500 na mavazi ya nyuki na kifaa cha kuvuna vumbi la Singida.

"Chanzo cha sumu ya nyuki kuuzwa ghali ni kwamba, kuna tafiti zinaendelea na zinaweza kuleta matunda itatibu kama sio kumaliza ugonjwa wa saratani na pili kuna kila dalili hii sumu ya nyuki ule ugonjwa wa UKIMWI inaweza kuwa kiboko yake," alisema.

Pinda alisema kutokana na hali hiyo, hawapotezi muda katika kumlinda nyuki ili kunufaika naye kwa kuwa kwa upande wa afya ni chakula kizuri na ni fursa ya uchumi.

"Tumlinde sana mdudu nyuki na wataalamu wanatuambia nyuki wakipotea leo ghafla maisha ya mwanadamu yatabaki ya mwaka mmoja tu. Unabaki unaanguka utafikiri umerogwa ndiyo maana tunashauri tumia angalau kijiko kimoja cha asali kwa kuwa kuna kila aina ya chakula ndani ya asali," alisema. Pinda alisema dunia nzima inahangaika na mdudu huyo kwa kuwa vyakula vingi duniani ili kupata mbegu kunatakiwa kufanyike uchavushaji ambao unafanywa na nyuki, kwani kwenye mazao yote asilimia 90 yanamtegemea nyuki.

"Ukienda Ulaya nyuki wakipotea kidogo tu inakuwa kilio kwa maana bila nyuki hakuna chochote ndiyo maana dunia nzima inamwangalia nyuki kwa jicho kali," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na mazingira mazuri yaliyoko Tanzania, ilistahili kuwa kinara wa uzalishaji wa asali duniani, lakini kiwango kinachozaliswa ni tani 35,000 tu.

Pinda alisema Tanzania imepewa heshima ya kuandaa mkutano mkubwa wa kidunia utaofanyika 2027 ambao utawashirikisha wadau zaidi ya 6,000 wa nyuki kutoka nchi 117.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kijiji cha Nyuki, Philemon Kiemi, alisema katika utafiti alioufanya wa miaka 12 amegundua mazao matano yanayotokana na nyuki tofauti na mwanzo ambapo wafugaji wa nyuki wanafahamu asali na nta tu.

Alitaja mazao ya nyuki mapya kuwa vumbi la Singida ambalo inasaidia nguvu za kiume na inauzwa Sh.laki 3 kwa kilo moja, maziwa ya nyuki yanauzwa Sh.milioni 12 kwa kilo,mkate wa nyuki Sh.300,000,gundi la nyuki Sh.milioni 3 na sumu ya nyuki ambayo inauzwa Sh.milioni 150 kwa kilo.

Kiemi alisema idadi ya makundi ya nyuki yaliyoko katika Mkoa wa Singida inafanana na idadi ya watu mkoani humo, lakini makundi yaliyoweza kukaa kwenye mizinga ni 240 tu na yaliyobaki yanakaa kwenye madari, mashimo, ardhini, magome ya miti, zahanati na shule. "Niwaombe wananchi kuendelea kuweka mizinga ili kuwanusuru nyuki wasikae kwenye zahanati,shule na pia watu wasikate miti badala yake wapande miti ambayo inapendwa na nyuki.

"Tunaamini kuwa, kama wafugaji wa asili wakipata vifaa vya kisasa kama vile mzinga wa Singida Techno Heifer na kuvuna mazao mapya kama vumbi la Singida pamoja na kupata vifaa vya kujikinga na nyuki wakati wa kulina asali sekta ya nyuki itapaa na kuwainua wananchi wengi nchini kiuchumi," alisema.

# Malalamiko 13,500 wananchi yamfikia Dk. Mwinyi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya malalamiko 13,517 yamepokewa katika mfumo wa Sema na Rais wa Zanzibar (SNR) katika kipindi cha miaka mitatu tangu kuanzishwa mwaka 2021.

Kati ya malalamiko hayo, 11,116 sawa na asilimia 82.6 yamefanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi na mengine 2,351 sawa na asilimia 17.4 yako katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya miaka mitatu ya mfumo huo ambao lengo lake ni wananchi kutoa kero zao kwa njia ya mtandao na kupatiwa ufumbuzi kwa muda mfupi kupitia taasisi husika.

Rais Mwinyi alisema pamoja na kutimiza miaka mitatu ya mfumo wa SNR, bado kuna kazi ya kufanya ili kuhakikisha unaleta mafanikio yaliyotarajiwa.

Kitengo cha SNR, alisema kina wajibu wa kuendelea kutoa elimu kwa kutumia njia mbalimbali kwa wananchi ili kuutumia vyema mfumo huo kwa madhumuni yaliyokusudiwa ya kutatua kero na changamoto zinazowakabili.

Alisema kuna haja ya watendaji wa kitengo hicho kuzidisha ushirikiano na wizara na taasisi zote hasa zenye idadi kubwa ya malalamiko ambayo yanakaa kwenye mfumo kwa muda mrefu bila ya kupatiwa ufumbuzi.

Rais Mwinyi aliagiza vijana wanaohusika na SNR wapewe ushirikiano wa kutosha katika kufanya kazi zao na pia, kuzingatia suala zima la utunzaji wa siri, huku akisema kuwa, anayaona masuala yote yanayowasilishwa katika mfumo huo.

Kiongozi huyo aliwatanabaisha viongozi na watendaji kuhusu taarifa zinazotumwa dhidi yao kuhusiana na masuala yaliyo kinyume na maadili ya uongozi yakiwamo yanayohusu uhusiano na kukosa uadilifu.

Alisema ni vyema viongozi na watendaji wa aina hiyo waache kuzitumia ofisi na dhamana zao kwa maslahi yao binafsi kwani ikithibitika serikali haitoacha kuwachukulia hatua.

Hata hivyo, Rais Mwinyi alisema wizara ambazo hazijafanya vyema, ziandae mikakati ya kuyafikia malengo ya kuanzishwa kwa mfumo wa SNR katika kuwatumikia wananchi.

Naibu Mkurugenzi wa Mfumo wa Sema na Rais, Haji Khamis Makame, alisema taasisi tano zimefanya vizuri katika kuyapatia ufumbuzi matatizo ya wananchi yaliyowasilishwa katika mfumo huo.

Akizitaja taasisi hizo ni Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar, ZSSF, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa , Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ na Wizara ya Maji na Nishati.

Kwa upande wa taasisi ambazo hazikufanya vizuri katika kutatua kero za wananchi ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema kitengo hicho kimetumia jumla Sh. bilioni 20.9 kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ya wananchi katika kuyapatia ufumbuzi matatizo

Hata hivyo, alisema miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana tangu kuanza kutumika kwa mfumo huo ni kuongezeka kwa uwajibikaji na ufanisi kwa watumishi wa umma pamoja na kupunguza urasimu katika sehemu za kutoa huduma.

## HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi ajifungua, atupa kichanga chooni

**Na Said Hamdani,** LINDI

MWANAFUNZI wa Kidato cha Pili, katika Shule ya Sekondari Mchinga, Wilaya ya Lindi, mkoani humo, (jina linahifadhiwa) mwenye umri wa miaka 17, amedaiwa kujifungua na kutupa kichanga katika shimo la choo.

Kichanga hicho kilichozaliwa wiki iliyopita kimeokolewa na mwananchi Ally Hussein, aliyekuwa anapita njiani karibu na choo hicho baada ya kusikia sauti ya mtoto.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Andrew Ngassa, alisema baada ya mwananchi huyo kusikia sauti ya kichanga chooni alitoa taarifa kwa wananchi na kufanikiwa kumwokoa.

"Askari walipofika eneo la tukio walikichukuwa na kukipeleka Hospitali ya Mkoa Sokoine iliyoko mjini Lindi kwa matibabu zaidi," alisema.

Ngassa alisema askari walipofanya uchunguzi walibaini michirizi ya damu iliyoanzia eneo la choo hadi nyumbani kwa mwanafunzi huyo.

Alisema baada ya mwanafunzi huyo kutekeleza tukio hilo alikwenda shuleni na kuendelea na masomo yake.

"Baada ya kubaini hilo askari walifika shuleni na kumkuta wakamchukua hadi kituoni kwa mahojiano na amekiri kutenda kosa," alisema ACP Ngassa.

Kaimu Kamanda alisema mama mzazi wa mwanafunzi huyo, Wepi Ibrahimu, alipoulizwa kuhusu mwenendo wa binti yake alijibu hakujua kama ni mjamzito na siku ya tukio alimwona akijiandaa kwenda shule kuendelea na masomo yake.

Alisema baada ya mahojiano na kukiri kosa mwanafunzi huyo amekabidhiwa chini ya uangalizi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii,huku taratibu za kisheria zikiendelea kuandaliwa dhidi yake.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Sokoine Mkoa wa Lindi, Dk. Alexanda Makalla, amekiri kumpokea kichanga hicho ambacho afya yake inaendelea kuimarika.

Mwanafunzi huyo alidai kuwa alitekeleza tukio hilo ili aendelee na masomo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah (wa pili kushoto), akizungumza na Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (kushoto), baada ya kufungua mjadala wa Dira ya miaka 50 ya chuo hicho, jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kulia) ni Makamu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Nasib Mramba. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mfanyakazi kampuni ujenzi afa gesti

**Na Said Hamdani,** LINDI

MFANYAKAZI wa Kampuni Lujuni Construction Ltd inayojihusisha na ujenzi wa barabara, Mahamudu Mbwana (44), amefariki dunia katika nyumba ya kulala wageni wakati akifanya mapenzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Andrew Ngassa, alisema jana kuwa Mbwana alikutwa amefariki dunia katika nyumba ya kulala wageni ya Another Coast iliyoko Kata ya Mikumbi, akiwa na rafiki yake wa kike aliyefahamika kwa jina la Gemina.

Alisema Mbwana ambaye ni mkazi Mbezi mkoani Dar es Salaam, alikutwa na umauti huo majira ya alfajiri baada ya kuanza kujihisi kuishiwa nguvu na kukoroma, ndipo mpenzi wake alipotoa taarifa kwa mhudumu wa gesti ambaye aliliarifu Jeshi la Polisi.

Baada ya askari kufika eneo la tukio, alisema walikuta tayari ameshafariki dunia na katika suruali yake walikuta dawa za kulevya aina ya bangi.

"Baada ya kukamilisha taratibu za kiuchunguzi, mwili wa Mbwana umekabidhiwa kwa mwajiri wake, Lufurano Ludovick (64), kwa utaratibu zingine," alisema.

Kamanda Ngassa alisema watu wengine wawili wamekufa katika matukio mawili tofauti, kwa kushambuliwa na wananchi kutokana na tabia za udokozi na mwingine kunywa sumu kwa madai ya hali ngumu za maisha.

Alisema matukio hayo yametokea Februari 27, mwaka huu na lingine Machi 4, mwaka huu. Ngassa amewataja marehemu hao, Erick Kilonzo (19) na aliyefahamika kwa jina la Bwanga (53), wakazi wa Kata za Mpilipil na Mlandege Manispaa ya Lindi.

# Watatu wawekwa kando tengua ya Rais

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi na utenguzi wa viongozi huku akimwondoa Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Richard Kiiza, ambaye amedumu katika nafasi hiyo kwa miezi mitano.

Ndani ya kipindi kisichozidi wiki moja, Rais Samia amefanya uteuzi na utenguzi wa viongozi katika ngazi mbalimbali zikiwamo za wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa.

Katika uteuzi na utenguzi huo, Rais Samia amewateua viongozi wapya wengine wakipandishwa, kuwahamisha na kuwaondoa katika nafasi zao kwa ahadi ya kupangiwa kazi nyingine au kutenguliwa kabisa.

Kiiza aliteuliwa kushika nafasi hiyo Oktoba 13, mwaka jana, na kabla ya uteuzi huo, alikuwa Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, bado hajateuliwa mtu wa kushika nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

Wengine waliokumbwa na tengua ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Damasi Mfugale, ambaye kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Ikulu uteuzi wake umetenguliwa na nafasi hiyo imechukuliwa na Ephraim Mafuru. Mfugale aliteuliwa Februari 3, mwaka 2023 kushika nafasi hiyo.

Kabla ya uteuzi huo, Mafuru alikuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).

Rais Samia amemteua Mhandisi Mwajuma Waziri kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Kabla ya uteuzi huo Mhandisi Waziri alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji.

Mhandisi Waziri anachukua nafasi ya Profesa Jamal Katundu ambaye uteuzi wake umetenguliwa akidumu katika nafasi hiyo kwa muda wa miezi saba.

Rais Samia amemteua Ally Gugu kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kabla ya uteuzi huo Gugu alikuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma.

Wateule wengine ni Kaspar Mmuya ambaye amekuwa Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma. Kabla ya uteuzi huo Mmuya alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Desemba 14, mwaka 2022, Rais alimteua kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kabla ya uteuzi huo Mmuya alikuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**FAUSTINE VALENTINE MOSHA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 529 BPQ** TOYOTA HILUX. CHASSIS **NO: LN1070004838.** ENGINE **NO: 3L2940363.** KWA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI: **PHQ/ARU/ARU/5666/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and administration Cause No 5127 of 2024**
**In the matter of the estate of the late JOSEPH MARTIN MILANZI of Msalato within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by MARIA SALUMU MWAYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 day of 3.... 2024

Dated at Dodoma this 13 day of 3.....2024

RESIDENT MAGISTRATE

RIPOTI MAALUM-2

# Simulizi 'mchongo' mabinti wa kazi wanaopokewa mijini

## -Wakimbia kuozeshwa, waangukia ukatili wa mabosi

**Na Waandishi Wetu**

SHERIA ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 inazuia utumikishaji wa watoto lakini mabinti wengi wa kazi mijini ni watoto na namna ya kuwapata ni 'michongo' mitupu.

Wadau wa eneo hilo waliozungumza na Nipashe wakiwamo mabinti wenyewe, wameeleza kwa kina namna ilivyo biashara hiyo, mtoto anavyoondolewa mikononi mwa wazazi wake hadi anapotumikishwa.

Serikali nayo haiko nyuma katika hilo imesema inatambua na imekuwa ikipambana na tatizo hilo na wapo baadhi ya watu wamefikishwa mahakamani.

**SIMULIZI ZA MABINTI**

Zawadi (si jina lake halisi) mwenye umri wa miaka 13, mwenyeji wa mkoa wa Kagera, aliingia Dar es Salaam Februari 26, mwaka huu, kwa ajili ya kufanya kazi za ndani baada ya bosi wake kutuma kijijini Sh. 150,000 kwa wakala wa biashara hiyo ili kutafutiwa msichana.

Katika mahojiano, mtoto huyo anasimulia kuwa mwaka jana aliacha shule akiwa darasa la sita baada ya viboko kuwa vingi kutoka kwa walimu wake, hivyo akaanza kutumikishwa kazi mbalimbali ikiwamo ya uyaya.

"Nilipoacha shule nikawa ninakaa nyumbani kwa mama wakati mwingine kwa bibi. Tumezaliwa watoto wanane, mimi ni wa sita kuzaliwa, nina wadogo zangu wawili mmoja anasoma.

"Ninakaa na mama. Wazazi wangu hawaishi pamoja waliachana. Tunaishi kijiji kingine na baba anaishi kingine na wake wengine. Kabla ya kuja hapa (Dar) nilikuwa ninafanya kazi ya uyaya kwa dada (anamtaja jina). Yeye anafanya kazi ya kudanga ana mtoto wa mwaka mmoja.

"Akienda katika madanga yake, anamwomba mama nikakae na mtoto wake. Akirudi alikuwa ananipa Sh. 1,000 ambayo nilikuwa ninanunua vitu vidogo au siku nyingine ninampelekea mama. Mama anafanya biashara ndogo sokoni," anasimulia.

Anasema maisha ya nyumbani kwao ni ya kawaida yakitegemea mlo mmoja au miwili kwa siku huku mama yake ambaye ndiye kila kitu, wakati mwingine hujishughulisha pia na kilimo.

"Mama ndiye anayenilea pamoja na wadogo wangu. Wakubwa wangu wengine wameolewa, kuoa na wengine wako na maisha yao. Umri wa mtoto wa kwanza sifahamu.

"Mama aliniambia nije huku (Dar) kwa ajili ya kufanya kazi za ndani. Mshahara sijui ni shilingi ngapi, sikuambiwa. Ninapenda kusoma lakini bado sijajua kusoma vizuri," anabainisha.

Bosi wa mtoto huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, mkazi wa Mwenge, anasema baada ya kumpokea na kumhoji alibaini changamoto



ni ugumu wa maisha na ndicho chanzo cha usafirishaji na utumikishaji watoto.

"Kama unavyomwona amelingana na watoto wangu. Nimejiuliza ni kazi gani ya kumpa afanye? Watoto wangu wanaamka asubuhi kwenda shuleni, je, yeye atabaki nyumbani kucheza au kuangalia TV? Hapana.

"Nimewasiliana na aliyenitumia ili amjulishe mzazi wake kuwa mtoto anarejeshwa anastahili kuwa shuleni, hivyo anaondoka usiku wa kuamkia kesho (Jumamosi iliyopita) kurudi nyumbani. Nimechelewa kumrudisha kwa sababu nilikuwa ninajikusanya kutafuta nauli yake," anasema.

Simulizi yake haitofautiani na ya Ninawajali (si jina halisi) aliyepelekwa Dar es Salaam mwaka 2022 akitokea mkoani Iringa akiwa na umri wa miaka 14.

Ninawajali ambaye anatokea kijiji cha Mgowelo, Kata ya Nyanzwa, Wilaya ya Kilolo, anasimulia kuwa alifika Dar es Salaam baada ya shangazi yake kutuma nauli kwa mama yake akitaka aende kuuza duka. Hata hivyo, alipofika alipelekwa kwa mtu maeneo ya Sinza Madukani kufanya kazi za ndani.

"Nikawa nafanya kazi ya kufua, kupika na kuwapeleka na kuwachukua watoto shuleni. Baadaye nikawa naenda kukata majani ya ng'ombe. Ilifika hatua nikawa sipewi mshahara ndipo nilipoacha na kurudi kwa shangazi. Kwa sasa ninauza chakula kwa mtu," anasimulia binti huyo ambaye anasema alifeli darasa la saba.

Mama mzazi wa binti huyo, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu mwishoni mwa wiki, alisema mtoto wake alimweleza mateso anayopata na kitendo cha kutopewa mshahara.

"Nilimwambia arudi nyumbani, akasema nimtumie nauli hajalipwa mshahara. Nilimwambia aende kwa shangazi yake wakati ninajipanga kutafuta nauli, arudi aje aolewe," anasimulia .

Simulizi nyingine ni ya Sarafina (si jina halisi) mwenye umri wa miaka (15), mkazi ya Nagulo Bahi, mkoani Dodoma. Anasema hofu ya kuozeshwa katika umri mdogo ndiyo inayowakimbiza nyumbani kwenda mijini kutafuta kazi za ndani au kwenye migahawa.

Binti mwingine anayefanya kazi za ndani jijini Arusha (jina limehifadhiwa), anasema mbali na kutumikishwa kazi ngumu, hupigwa na mwajiri wake amewahi kumchoma na pasi kisa alikuwa hajafua nguo vizuri.

**SAFARI KWENDA MIJINI**

Baadhi ya watoa huduma za usafiri wa mabasi ya mikoani, wamefunguka ugumu waupatao pindi wanapokabidhiwa watoto wadogo wenye umri kati ya miaka 13 hadi 17 kuwasafirisha kwenda mijini.

Richard Goodluck, kondakta wa mabasi ya Tilisho, anafunguka mbinu ambayo baadhi ya wazazi au madalali hutumia wanapowasafirisha watoto ni ya kukata tiketi mapema .Baada ya kufika, humkabidhi kwa kondakta na kumlipa fedha kidogo ili asishuke njiani.

"Changamoto ni pale umekubali unafika mjini, anayetakiwa kumpokea hujamwona, unalazimika kuzunguka naye mpaka achukuliwe. Kinyume cha hapo kesi umeinunua. "Wako ambao unakabidhiwa hajapewa fedha za kujikimu njiani, inabidi uingie mfukoni mnunulie japo kitu kidogo kupoza njaa," anasema.

Dereva wa basi la Kampuni ya Masalu, Abdahallah Kazinza, anasema: "Kuna wakati tunalazimika kurudi nao walikotoka kutokana na kutowaona wenyeji wa kuwapokea au wakati mwingine hulala kwenye gari."

**WAKALA AFUNGUKA**

Mmoja wa mawakala wa mabasi ya Kandahar, yanayofanya safari kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa na Singida, ambaye hakutaka jina lake liandikwe, anasema mabinti wengi wadogo kutoka mikoa ya Mwanza, Singida, Shinyanga na Simiyu wamekuwa wakisafirishwa kwenda mijini kufanya kazi za ndani.

"Wengine wanatelekezwa stendi za mabasi. Kijana akiona anamlaghai wengine wanaishia kwenda kuwafanyisha biashara za ngono,"anasema.

Msafirishaji mwingine katika stendi ya mabasi Shinyanga (jina linahifadhiwa), anasema amekuwa akisafirisha mabinti baada ya kukabidhiwa na mwanamke ambaye hakumtaja jina.

"Huwa tunawasiliana kwa simu anawapakia katika gari wakifika hapa ndipo ninawasafirisha kwenda Dodoma au Dar es Salaam. Kwa wiki ingawa si zote, huwa ninasafirisha hadi watoto watatu. Kwa mwaka huu, nimewasafirisha 10 umri wao ni ule wa kuwa shuleni," anasema.

MABOSI

Rehema Renatus, mkazi wa Moshi, Kilimanjaro anasema: "Nimewahi kutuma Sh. 100,000 nikaambiwa binti anatoka Mwanza Vijijini na ni mkubwa, kumbe alikuwa Pasua (Moshi).

"Alikaa kwangu kwa siku 14 tu, akaomba kuondoka akisema wazazi wake ni wagonjwa. Nilibaini baada ya muda kwamba ulikuwa mchezo. Hii ni biashara ya mtu anachukua nauli na kuwauza, halafu wanafundishwa wakifika kazini baada ya muda wafanye ukorofi ili warudi,"anasimulia.

Mkazi wa Mwanza, Gladness Godfrey, anasema baadhi ya watoto vijijini hawapendi kwenda shule kwa sababu mbalimbali ikiwamo umbali wa shule, ugumu wa maisha nyumbani, makundi rika huku wazazi wao wakishindwa kumudu gharama za shule za bweni.

"Tunajua haki ya mtoto ni kupata elimu. Wako wanaolazimishwa kuolewa katika umri mdogo, wengine wanalazimika kutoroka nyumbani au kutoroshwa na kuletwa mijini kutumikishwa wakisahau nayo ni ukiukwaji wa haki ya mtoto," anasema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Karume, Kata ya Mnadani jijini Dodoma, Matwiga Kyatya, anasema amewahi kupokea kesi ya mtu kuletewa binti mwenye umri wa miaka 13 kutoka Kagera kwa ajili ya kufanya kazi za ndani kwa mshahara wa Sh. 50,000 kwa mwezi na hatua zilizochukuliwa ni pamoja na mzazi wake kuitwa, kuonywa na kukabidhiwa mtoto.

**KAULI YA SERIKALI**

Katibu wa Sekretarieri ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Separatus Fella, anasema tatizo la usafirishaji haramu binadamu lipo.

Anasema hivi karibuni lilikuwapo mkoani Kigoma ambako watoto husafirishwa kutoka Burundi kwenda kutumikishwa kazi mbalimbali zikiwamo za ndani.

"Wengine wanatumikishwa majumbani au mitaani. Tatizo hili limevuka hadi kwenye miji mikubwa kama Dar es Salaam. Wengine wanawachukua watoto wenye ulemavu kuwatumikisha mitaani," anasema.

Fella anataja takwimu za kuzuia usafirishaji haramu binadamu kipindi cha Julai hadi Desemba, 2023 ambazo zinaonyesha wahalifu 11 miongoni mwao waliosafirisha watoto walikamatwa na kesi tatu zilifunguliwa na zinaendelea kusikilizwa.

"Waathirika 99 waliokuwa chini ya umri wa miaka 18 waliokolewa. Waathirika hawa waliokolewa mikoa mbali mbali ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Kigoma na Zanzibar. Hawa walikuwa wakitumikishwa kazi za majumbani, biashara ya ngono, kuchunga mifugo, kulima mashambani na kuomba mitaani," anasema.

Anasema mtu yeyote akipatikana na hatia ya kusafirisha mtoto au mtu mwenye ulemavu, atafungwa kifungo kisichopungua miaka 30 na kadri mahakama itakavyoona inafaa atalipa faini isiyopungua milioni 50, lakini isizidi milioni 300.

Fella alisema mwaka 2008 Tanzania baada ya kuridhia mikataba ya kimataifa, ilitungwa Sheria ya mwaka 2008 ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu ambayo katika kudhibiti vitendo vyote vya usafirishaji haramu wa binadamu.

"Baada ya kutungwa iliwekwa adhabu kwamba mtu akipatikana na hatia anaweza kufungwa kifungo au kulipa faini au vyote kwa pamoja.

"Hii faini ilikuwa kwa makosa ya usafirishaji watoto ilifikia hadi zaidi ya Sh. milioni 150 na kifun-

INAENDELEA UK. 5

AGNETHA BAHIGWE



Jengo la kuhifadhi maiti la Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma. **PICHA: BMH**

# Binti wa miaka 24, 'jembe' la kutegemewa mochwari

**Na Mwandishi Wetu**

IMEZOELEKA wanaofanya kazi kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti (mochwari) wengi wao ni wazee, tena wanaotumia vileo vikali.

Hali ni tofauti kwa Agnetha Bahigwe, anayefanya kazi kwenye mochwari ya Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma.

Agnetha (24) ni mwanamke wa kwanza kufanya kazi kwenye chumba cha kuhifadhi miili cha Hospitali hiyo ya Rufani ya Kanda ya Kati, akiwa amefanya kazi hiyo kwa saa 7,244 katika miaka mitatu kazini ukiondoa siku za likizo ya kila mwaka.

"Si kweli kwamba tunaofanya kazi kwenye vyumba vya kuhifadhi miili tunapaswa kunywa pombe au kuvuta bangi ili kutekeleza majukumu yetu," anaeleza binti huyo.

Agnetha, mtoto wa nne kati ya sita wa Mzee Bethram Bahigwe na Elizabeth Jackson wa mkoani Kigoma, amesomea kazi hiyo katika Chuo cha New Mafinga Health & Allied Institute (NeemaUhai) kilichoko Mafinga, Iringa.

Anaeleza kitu ambacho anakumbuka zaidi katika majukumu yake tangu alipoanza kazi BMH miaka mitatu iliyopita, ni siku aliyopokea mwili uliopata ajali ya gari.

"Wakati nilipokuwa ninahitaji kuhifadhi mwili nikakuta sehemu ambayo ameumia kichwani ubongo upo nje, hiki kitu kilinisumbua sana kichwani," anasimulia.

Kitengo cha mochwari ya BMH kina majokofu yenye uwezo wa kuhifadhi miili 36 na hospitali kupitia watendaji wake, akiwamo Agnetha, ina jukumu la kutoa ushauri kwa wafiwa jinsi ya kuhifadhi mwili wa mpendwa wao. Agnetha anasema majukumu yake yanaanza kwa kukagua jengo mara tu anaporipoti ofisini.

"Baada ya kukagua jengo, ninakagua majokofu ya kuhifadhi miili, na miili ambayo imehifadhiwa pamoja na kukagua 'temperature' (hali joto) kwenye majokofu yenye miili," anasema.

Msimamizi wa Chumba cha Kuhifadhia Miili cha BMH, Paschal Mashauri, anasema hakuna changamoto yoyote anayoipata kutoka kwa Agnetha.

"(Agnetha) ni mtu anayetoa ushirikiano mkubwa wakati tunatekeleza majukumu yetu ya kiofisi, anakuja shifts (zamu) zote tatu tunazopangiwa, iwe asubuhi, mchana au usiku," anasema msimamizi wake wa kazi.

Agnetha, mama wa watoto wawili (mkubwa ni wa kiume mwenye umri wa miaka sita na mdogo wake wa kike mwenye umri wa miezi tisa), hakuwa tayari picha yake itumike gazetini kutokana na hofu ya unyanyapaa wa jamii dhidi ya watu wanaofanya kazi mochwari.

Anasema baba yake mzazi ambaye ni nesi mstaafu, ndiye aliyemshawishi kusomea usimamizi wa mochwari. Hakuna mwingine katika familia yao anayefanya kazi hiyo anayoitaja ajira zake ni za uhakika.

"Ni kazi ya kawaida kama kazi zingine ambazo watu wengine wanafanya. Darasa letu tulikuwa 19; wengine sasa wameajiriwa Mbeya, Morogoro na maeneo mengine nchini. Kama kuna binti mwingine anaona anaweza kuifanya, akasome," Agnetha anasema. Kuhusu tatizo la kuchanganya maiti ambalo limewahi kuikumba Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mara kadhaa, Agnetha anasema kwao (BMH) halijawahi kutokea, akisisitiza "kila tunapotoa mwili, lazima ndugu aingie kuthibitisha".

# Simulizi 'mchongo' mabinti wa kazi wanaopokewa mijini

INATOKA UK. 4

go hadi miaka 10, lakini mwaka juzi serikali iliona haitoshi ikafanya mabadiliko, ikaondoa faini kwa kuwa, watu walipokutwa na hatia walikuwa na uwezo wa kuilipa.

"Kwa sasa mtu akipatikana na hatia ni kifungo na faini inakuwa ni nyongeza endapo mahakama ikiamua kufanya hivyo," anafafanua.

Alitaja mikoa mingine yenye changamoto ya kusafirisha watoto mijini ni Simiyu, Kahama na Shinyanga ambao hupelekwa kwenda kutumikishwa katika shughuli mbalimbali.

**CHANGAMOTO**

Fella anasema; "Changamoto ya makosa hayo ni namna ya kudhibitisha kosa lililotendeka. Ukimkuta mtu mfano, yupo na watoto 30 ili udhibitishe ni unyonyaji wanakwenda kutumikishwa kidogo inakuwa ngumu.

"Sasa hivi tumefanya mabadiliko ya sheria yapo mapendekezo mengine yanakuja lengo ni kama mtu atakutwa na watoto wadogo hatutasubiri kudhibitisha hilo tendo la unyonyaji, tutaonyesha umejaribu kutenda kosa hilo."

Anasema jambo lingine ni uelewa na ushahidi kwa kuwa watoto wanapookolewa hawawezi kupelekwa mahakamani na kesi kuisha siku moja, hivyo kesi ikiendelea katikati kunakuwa na uvurugaji wa kesi.

"Kwa kuwa vitendo hivi huwa vya kimtandao, baadhi hujaribu kuvuruga ushahidi kwa kutishia mashahidi kuwa watawaua endapo watakwenda mahakamani kutoa ushahidi," anaongeza na kubainisha kuwa changamoto hizo zinafanyiwa kazi ili kusaidia kudhibiti vitendo hivyo na wahusika kupata haki.

## Murilo atoa somo ajira za madereva

**Na Joseph Mwendapole**

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Murilo, amezitaka kampuni za usafiri mtandaoni kuajiri vijana wenye sifa ya kudadisi abiria wanaowabeba kwa maswali yenye mwelekeo wa kutambua masuala ya usalama.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa huduma ya taxi mtandaoni maarufu kama SUKA.

Murilo alisema kampuni zinazotoa huduma za usafiri mtandaoni ni mdau muhimu sana kwa serikali kwa masuala yanayohusu usalama kwani wanahudumia watu wengi tofauti.

"Unapoingia kwenye kutoa huduma kama hii moja kwa moja wewe ni wakala wa serikali lazima uwe mdadisi kwa abiria unaowabeba siyo kwa maswali yenye maudhi lakini maswali yenye mwelekeo wa kutambua masuala ya usalama," alisema.

Alisema kuna Kampuni zilizokuwa zinatoa huduma zinazofanana na SUKA, hivyo kuwataka wamiliki wa kampuni hiyo kufuatilia kujua walifanikiwa kwa kiwango gani na walikwama wapi wakati wa kufanya shughuli zao.

"Fuatilieni mjue kumbukumbu za kampuni hizo zikoje kwenye mamlaka zilizofanya usajili wake na wananchi ambao walikuwa wanapata huduma hizo wanazungumziaje kampuni hizo ili mpate mwelekeo sahihi wa kazi zenu," alisema.

Murilo alisema anaamini wamiliki wa kampuni ya SUKA wamefanya utafiti na kuamua kuingia kwenye utoaji wa huduma hiyo wakiwa na malengo makubwa ya kuboresha zaidi huduma hiyo kuhakikisha hakuna malalamiko ya wateja.

Kamanda Murilo alisema miongoni mwa vitu vilivyokuwa vikilalamikiwa na wateja kwenye kampuni zilizokuwa zinatoa huduma kama hiyo ni tabia zisizo ridhisha za watu waliokuwa wakiendesha vyombo vya usafiri.

"Tabia zile zilishusha heshima ya huduma hiyo na watu walikuwa wakipata mrejesho wa lugha wanazopata kutoka kwa wahudumu wale, tabia ni pamoja na uvaaji ukihudumia watu lazima uvae mavazi ya heshima," alisema

Aliwataka kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya namna ya kutoa huduma hiyo ili kuhakikisha watoa huduma wanakuwa waadilifu kwa wateja na kuondoa malalamiko.

Ofisa Mawasiliano wa SUKA , Luciana Mwambinga, alisema waliamua kuanzisha huduma hiyo baada ya kuona heka heka za maisha ya kila siku na mahitaji ya usafiri hasa kwa watu wasio na usafiri kwa kutengeneza daraja linalofanikisha mawasiliano kati ya watoa huduma na watumiaji kwa urahisi.

Alisema SUKA ni mfumo unaowaunganisha abiria na madereva kwa urahisi, ufanisi, usalama zaidi na kwa gharama nafuu ambapo wameboresha zoezi zima la upatikanaji wa usafiri kupitia mtandao kati ya abiria na watoa huduma ya usafiri.

"Tunatambua kuwa abiria na dereva wote wanahitaji mazingira bora yenye ufanisi na usalama ili waweze kufanya shughuli zao vyema na kwa kuzingatia hayo SUKA imelenga na inapatikana kwa watumiaji wote wa usafiri," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi Waziri kuzuia uagizaji wa nondo nje unastahili pongezi

**TANZANIA** imekuwa mwagizaji wa bidhaa mbalimbali nje ya nchi kutokana na kutokujitosheleza kwa bidhaa zinazozalishwa nchini. Hatua hiyo imesababisha serikali kutumia mamilioni ya fedha za kigeni katika uagizaji huo, hivyo kuifanya sekta ya fedha kutokuwa himilivu.

Miongoni mwa bidhaa ambazo zimekuwa zikiagizwa kutoka nje ni pamoja na nguo, mafuta ya kupikia, sabuni, sukari, dawa za mifugo na za binadamu, vijiti vya meno, viberiti, vifaa vya ujenzi na vinywaji. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni ama viwanda vya ndani kukosa uwezo wa kuzalisha kwa wingi bidhaa zinazohitajika au kutokuwapo kabisa kwa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa husika.

Kuwapo kwa tatizo hilo, kama ilivyokuwa katika uhaba wa mafuta ya kula na sukari, serikali ya awamu ya tano katika kipindi chake cha kwanza, ilichukua hatua madhubuti kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa hizo kwa viwanda vya ndani unakuwa mkubwa.

Katika suala la mafuta, mkakati uliandaliwa kuongeza uzalishaji wa alizeti na michikichi na kwa upande wa sukari, mkazo ulikuwa katika upanuzi wa viwanda vilivyopo na ujenzi wa viwanda vipya.

Aidha, kutokana na sera ya maendeleo ya viwanda katika serikali ya awamu ya tano kwa ajili ya kukuza uchumi na kuongeza ajira, imeshuhudiwa ongezeko la viwanda vya bidhaa mbalimbali kwenye maeneo kadhaa nchini. Hatua hiyo imesaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa, hivyo kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.

Moja ya maeneo ambayo uzalishaji wa bidhaa umeongezeka ni katika vifaa vya ujenzi hasa nondo na mabati ambavyo vimesaidia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa miradi kadhaa ya kimkakati kama vile Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere katika Mto Rufiji na reli ya kisasa (SGR).

Kutokana na kuwapo kwa uzalishaji ambao unatosheleza mahitaji ya ndani na hata ziada kuuzwa nje ya nchi, juzi Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hakuna haja tena kwa serikali na taasisi zake kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Prof. Mkumbo alitoa kauli hiyo alipotembelea kiwanda cha Lodhia, kinachotengeneza nondo, mabati na bidhaa za plastiki ambacho kwa sasa kinazalisha tani 18,000 za nondo na matarajio yake ni tani milioni moja kwa mwaka. Kutokana na uwezo wa kiwanda hicho na vingine, alisema nchi i najitosheleza kwa nondo, hivyo hakuna ulazima wa kuagiza bidhaa kama hizo kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani.

Uamuzi huo ni mwafaka kwa sababu pamoja na kulinda viwanda vya ndani, utasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika kuagiza bidhaa kama hizo nje ya nchi.

Licha ya kutangaza huko, ni vyema sasa jambo hilo likapata baraka za serikali kwa kuweka sheria ambayo itasaidia kuzuia uingizaji wa bidhaa ambazo zinapatikana nchini hasa nondo kama alivyotamka Waziri.


Kuwapo kwa bidhaa za kutosha katika nondo na mabati, kunaonyesha ishara kwamba Tanzania inaanza kupiga hatua katika uchumi hasa kutokana na uwekezaji wa viwanda katika maeneo mbalimbali.

Ni wakati mwafaka sasa serikali kufanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji ili kubaini bidhaa zinazozalishwa kwa kuvuka malengo yaliyowekwa kulingana na mahitaji na hatimaye kutangaza hatua za kuzuia uingizaji wa bidhaa kutoka nje.

Hatua hiyo itawezesha kuimarisha uchumi pamoja na uimara wa sarafu ya nchi.

Kwa ujumla, hatua ya Waziri kutangaza kuwa nchi inajitosheleza kwa vifaa vya ujenzi inapaswa kupongezwa na kuungwa mkono kwa maendeleo ya nchi. Kazi iliyobaki sasa ni kuzuia au kudhibiti uingiaji wa bidhaa hizo kutoka nje ili kulinda viwanda vya ndani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Magufuli nyota iliyozimika, ametimiza ndoto ya Nyerere

Na Sabato Kasika

**LEO** ni kumbukumbu ya miaka mitatu ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, aliyeonekana kwenye jamii kama kiongozi mwenye uamuzi mgumu.

Katika uongozi wake, alifanya uamuzi mgumu katika mambo mengi ikiwamo kuwatumbua baadhi ya wataule wake ambao walibainika wanakwenda kinyume cha kile alichotarajia wakifanye, kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Lakini uamuzi mgumu zaidi alioufanya ni kuhamisha makao makuu ya nchi kwenda Dodoma, uamuzi uliokuwa unasuasua tangu mwaka 1973 wakati wa utawala awamu ya kwanza.

Tangu mwaka huo, Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, alianza mchakato wa kutaka kuhamishia makao makuu ya nchi Dodoma lakini hadi anang'atuka katikati ya miaka ya 1980, hilo halikutumia.

Ikafuata awamu ya pili ya uongozi wa nchi hadi ya nne, awamu hizo nazo zilipita bila kutekeleza ndoto hiyo ya Baba wa Taifa.

Lakini baada ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli kuingia madarakani, suala la makao ya nchi lilipewa msukumo mkubwa.

Taasisi na wizara zilihamia huko kisha yeye Rais akawa ni wa nwisho kutoka Dar es Salaam baada ya kujiridhisha kuwa kila kitu kimekwenda sawa

Baadhi ya watu waliona kama uamuzi huo ni jambo lisilowezekana, hasa kutokana na kwamba lilikaa miaka mingi bila kutekelezwa.

Lakini Dk. Magufuli alipotangaza uamuzi huo Julai, 2016 ikiwa ni zaidi ya nusu mwaka tangu aingie madarakani, alisimamia hadi ukatekelezwa.

Mwenyewe alisema lengo kuu lilikuwa ni kutimiza ndoto ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoitoa mwaka 1973 ya kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi.

Alisisitiza kuwa: "Jukumu langu lilikuwa kutekeleza ahadi ya Mwalimu Nyerere na nilipata nguvu baada ya kukumbuka kuwa ziko nchi nyingi tu duniani zikiwamo nchi za Afrika kama Nigeria na Ivory Coast ambazo zilihamisha makao makuu ya nchi katika kipindi kifupi."

Baada ya makao makuu ya nchi kuhamia Dodoma, kuna miradi mbalimbali imejengwa imekamilika ikiwamo ofisi za Ikulu ya Chamwino.

Miradi mingine inaendelea kujengwa kuanzia majengo ya mji wa serikali, ujenzi wa uwanja kubwa wa michezo, ujenzi wa barabara mbalimbali, ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa, bandari kavu, kwa kuwa jiji la Dodoma lina kituo kikuu cha reli ya kisasa (SGR), kituo cha afya katika mji wa serikali.

Kwa ujumla ni kwamba kuna ujenzi wa miradi mingi, hasa baada ya uamuzi mgumu wa Rais Dk. John Magufuli alioufanya alipoingia madarakani baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Uamuzi wake mgumu ambao haukufanywa na watangulizi wake, umeufanya mji wa Dodoma kuwa jiji ambalo linazidi kukuwa kila kukicha kutokana na fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo.

Ninaweza kusema kwamba, mfupa uliowashinda viongozi wengine kwa miaka 43, yeye aliuweza na kutimiza ndoto ya Mwalimu Nyerere.

Tunapomkumbuka Kwa mengi, miongoni mwake hilo la kuhamisha makao makuu ya nchi kwenda Dodoma, tofauti na ilivyokuwa awali wakati ofisi zote za kiserikali zilikuwa Dar es Salaam.

Baada ya kifo chake, awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeendeleza lengo hilo hadi kufikia kukamilisha ujenzi wa Ikulu ambayo tayari inatumika. Hivyo ndivyo Magufuli alivyotimiza ndoto ya Mwalimu Nyerere.

FIKRA MBADALA

# Buriani Santus Mtsimbe, matendo yako yataishi daima



Pascal Mayalla

KUNA usemi kwamba mtenda mema hulipwa mema, vivyo hivyo kwa mtenda mabaya. Ni maneno yanayotukumbusha namna ya kuishi maisha mema kabla ya kwenda mbele za haki huku tukitambua kuwa maisha yetu ya hapa duniani ni ya kitambo tu kama yanenavyo maandiko matakatifu.

Wako wengi ambao miaka mingi imepita tangu wafariki dunia lakini kutokana na mema waliyoyafanya katika jamii au taifa, wanaendelea kukumbukwa. Kwa maneno mengine, matendo yao yameacha alama isiyofutika kwa miaka mingi na watakumbukwa na vizazi vingi.

Leo tunamsindikiza Mtanzania mwenzetu, Sanctus Mtsimbe ambaye japo ni Mtanzania wa kawaida, mwanachama wa mtandao wa Jamiiforums. Japo ametangulia, nyuma ametuachia hazina kubwa ya maarifa kwa maandishi na video zake.

Taarifa ya msiba huu, ilitolewa na Mtendaji Mkuu wa Jamiiforums, Maxence Melo akisema: "Wakuu, nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kufariki dunia kwa ndugu yetu na mwanachama wa JamiiForums, Sanctus Mtsimbe, mchana wa Machi 13, 2024.

Mtsimbe alikuwa Rais wa Kwanza wa Mtandao wa Wanataaluma Tanzania (TPN). Hadi anafariki dunia alikuwa Meneja wa Wananchi Group Tanzania ambao ndio wamiliki wa Zuku, SimbaNet na kampuni zingine.

Pia alikuwa mjasiriamali na mmiliki wa kampuni kadhaa binafsi na mjumbe wa bodi katika taasisi kadhaa za umma na binafsi. Mtsimbe alikuwa mwanazuoni mzuri, mbobezi, mbunifu na mzalendo wa kweli kwa nchi yetu. Alikuwa swahiba wangu katika baadhi ya miradi yake.

Huyu ndiye aliongoza ile kampeni ya kumuenzi aliyekuwa mbunge wa viti maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA),Regia Mtema, aliyefariki dunia kwa ajali ya gari Ruvu Darajani kwa kumwandikia kitabu. Huyu ndie alimbeba mwanachama mwingine wa JF, Le Mutuz pale ofisini kwake. Pia alinikaribisha ofisini kwake na kuitumia studio yake wakati wowote.

Kuna baadhi ya vitu mimi na Mtsimbe tulifanana na kuna vingine tulitofautiana. Tulifanana kupenda vitu vizuri, gari zuri, suti nzuri, suti kali na kushirikiana na watu wazuri, wakiwamo wasanii maarufu.

Japo mimi ni Msukuma na sisi Wasukuma tunasifika sana kwa ushamba. Lakini naomba kukiri kuwa japo mimi ni Msukuma wa mjini, niliyezaliwa mjini, nikasomea mjini, ni mshamba wa Kisukuma wa kuchanganyikiwa na 'vitu vyeupe'. Hilo nakiri wazi kabisa.

Mwaka 2007 kuna tukio fulani pale British Council, Mtsimbe alikuwa anafanya wasilisho kuhusu SimbaNet na mimi nikachangia kitu. Wakati tunatoka, aniuliza Kiti Moto kimefia wapi? Tuonane tukifufue hatimaye tukaagana. Nilipomwangalia, akavuka barabara hadi kwenye sehemu aliyokuwa ameegesha gari lake aina ya Range rover Sport pale CRDB Tawi la Holland House. Nilisimama nikimkodolea macho mpaka anaishia.

Toka hapo tukaanza urafiki, akanikaribisha SimbaNet, tukaa chini kuanzisha studio, akaanzisha Jason Production, alinikaribisha kwenye studio yake na niliitumia bure pale TANCOT House wakati nikiwa Mtaa wa Mkwepu.

Wakati wa kipindi kile cha kukaza kwa vyuma, mimi vilinikazia sana hadi vikaumana, hivyo kulazimika kufunga ofisi ya Mkwepu. Huyu jamaa alinibeba kwa muda pale ofisini kwake, ndipo nikagundua kumbe yale makeke yote na ubabe wa Le Mutuz, jeuri ile huyu jamaa ndiye alikuwa mfadhili na mhifadhi mkuu wa LE MUTUZ SUPER BRAND.

Tukakutana JF msiba wa Regia Mtema, akaongoza kampeni ya kumwandikia kitabu. Jambo lingine nililoligundua ni kwamba Mtsimbe alikuwa mtu mwenye ushawishi mkubwa. Hiyo ni baada ya kushinda zabuni ya kulitangaza Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kupitia kampeni ya 'Wekeza Inalipa', hivyo akanikaribisha tukaungana kwa ajili ya utekelezaji.

Kwenye hiyo tenda ya DSE mimi ndio nilikuwa mtangazaji kiongozi, nikapewa jukumu la kwanza kuwafundisha watangazaji wasaidizi. Watangazaji hao ni mabinti watano mastaa wa Bongo Movies. Hao mabinti wote walikuwa 'single', halafu mwalimu mwenyewe familia yake inaishi Marekani. Ulikuwa mtihani mkubwa kwangu lakini Mtsimbe alikuwa mwadilifu wa hali ya juu.

Baada ya project ya DSE kukamilika akafungua TV yake. Pia Mtsimbe aliasisi 'JF Get Together' na kunifanya kuwa MC.

Huyo ndiye Mtsimbe ambaye hakika alikuwa mtu wa watu. Pamoja na kwamba amtengulia mbele ya haki na leo tutamhifadhi katika nyumba yake ya milele, ataendelea kukumbukwa kwa mambo kadhaa lakini yafuatayo kwa uchache;-

Kwanza, alisisitiza 'connectivity', watu wajiunge na makundi mbalimbali na kupitia kujiunga huko, aliamini kila mtu anaweza kufanya kila kitu kwa kujiunga na wengine, hivyo kuunganisha uwezo na kutenda. Kupitia mfumo huo, ofisini kwake alisaidia watu wengi kushinda zabuni za kazi mbalimbali zilizokuwa zikitangazwa.

Pili, alisisitiza afya bora. Aliamini kwamba ili ufanikiwe ni lazima uwe na uwezo wa kufanya kazi, hivyo alisisitiza sana afya bora. Alikuwa hali ovyo ovyo, hanywi pombe, havuti sigara. Kwake jambo la muhimu lilikuwa kazi tu, akaandika kitabu cha jinsi ya kuondoa kitambi

Tatu, alichukia umasikini na kusisitiza utajiri, hivyo ametuachia makala nyingi za kuondoa umasikini na kupata utajiri.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, alipenda vitu vizuri, wakiwamo warembo. Kuna wanaume na mababa wengi wanapenda warembo. Ukweli ni kwamba watu hao si kwamba wanawapenda warembo hao ili wawasaidie bali wawatumie kwa manufaa yao. Mtsimbe aliwapenda warembo kwa dhati ili kuwasaidia na si kuwatumia. Kwa kweli amewasaidia wengi.

Buriani Komredi Santus Mtsimbe, vita umevipiga, mwendo umeumaliza, imani umeilinda.

**Bwana alitoa, Bwana Ametwaa, Jina la Bwana na Lihimidiwe.**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kuweni wakweli msimzingue Rais wetu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

BAADHI ya familia zenye ukwasi na watoto wengi, huwa na utaratibu wa kupangiana majukumu ya nyumbani hususan kwa wale ambao hununua mahitaji kwa jumla na si rejareja kama walalahoi.

Hutokea katika familia hizo, mtoto mmoja akapangiwa jukumu la kusimamia stoo ya chakula na kuhakikisha kinatoka kimahesabu na kwa ruhusa yake.

Mtoto huyo ndiye hutoa taarifa kwa msimamizi mkuu wa stoo ambaye mara nyingi huwa ni mama, kwani ndiye mara zote hujua ni chakula gani kipo na kwa kiwango gani na kipi hakipo kinastahili kuongezwa.

Inaweza kutokea nyakati msimamizi huyo wa stoo akaingiwa tamaa na kutumia vibaya nafasi yake kwa kuchomoa kidogo na kugawa au kuuza kwa watu wengine kutokana tu na ushawishi na si ukata.

Lakini inapotokea hivyo, uhakikisha msimamizi mkuu hajui na atajitahidi kumdanganya ili asibaini upungufu wa ghafla mpaka ifike siku ambao ni ya kufanya ununuzi mwingine wa mahitaji.

Kuna wakati mama anaweza kusikia watoto wengine walio kwishabaini njama za ndugu yao wakinong'ona kuhusu hali hiyo na hivyo mama kuingiwa na udadisi na kwa kuwa ni msimamizi mkuu anakuwa na ufunguo wake.

Lakini kabla hajafanya ukaguzi wa kushitukiza, msimamizi mtoto machale yanamcheza na kujipeleka kwa mama yake na kumwambia mambo yote yako shwari na asiwe na tatizo lolote, kwani anasimamia vizuri.

Na hapo humsifia kuwa usimamizi mkuu anaoufanya, unasababisha hali ya matumizi nyumbani kuwa mazuri na hakuna kilichotetereka na maisha ni mazuri kutokana na hatua hiyo. Mama anapokataa kushawishika, huamua kujitosa stoo na kukuta mambo yakiwa mrama na kupigwa na butwaa na kumkaripia mwanawe kwa uongo anaompa kwa maslahi binafsi na kuwataka wengine kutomwiga na kuwa makini katika mambo yao.

Hiyo huwa mwanzo wa kukosa imani kabisa na mwanawe huyo na wakati mwingine kumfanya afikirie kusimamia mwenyewe mambo yake ili siku moja asijechekea nyani na kuishia kuvuna mabua.

Nimekuwa nikifuatilia sana uamuzi wa Chifu Hangaya, hasa wa kupangua wasaidizi wake na wakati mwingine kuwahamisha au kuwatumbua kwa kukosa usimamizi imara wa nafasi zao, hususan katika kupambana na kero za wananchi.

Hutokea wakati mwingine baadhi ya wasaidizi wake kumdanganya, wakijua kuwa nchi hii ni kubwa yenye zaidi ya watu milioni 61, asioweza kuwafikia wote kirahisi kama asivyoweza pia kuzunguka kila kona ya nchi hii.

Hivyo mmoja wa wasaidizi hao huweza kusimama jukwaani na hata akiwapo Chifu mwenyewe na kuhanikiza: "Mama unapiga mwingi na ndiyo sababu wizi hakuna serikalini na ndiyo maana maendeleo yanaonekana.

"Rais umedhibiti wizi wa fedha na sasa hakuna wizi serikalini." Lakini katika muktadha huo huo, Chifu naye anapata nafasi na kuzungumzia masuala ya uchumi wa nchi na kuliambia Taifa: "Kuna mtandao unaiba fedha za Serikali."

Chifu Hangaya kulibaini hili na kulisemea, ni dhahiri baadhi ya wasaidizi wake wanamzunguka na kumdanganya na ndiyo sababu juzi wakati anaapisha wapya, aliwambia anajua kinachoendelea huko waendako na hivyo wakafanhye udhibiti.

Lakini hili likitazamwa kwa kina, linadhihirisha jinsi wasaidizi hao walivyomzoea wakijua hatawafanya lolote zaidi ya kuwatoa sehemu moja na kuwapeleka nyingine nao kuendelea kunoa meno na makucha na kurarua na kuchakura zaidi.

Halafu inashangaza, kuwa wengi wanaofanya hivi ni wanaosikika hata kwenye hotuba zao katika kila aya au mstari, wakimtaja Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan, kafanya hiki, kafanya kile, kaleta hiki, kaleta kile.

Ni hao hao utawasikia tumpongeze kwa kuleta pesa, chakula, magari, barabara, madaraja, hata mvua! Wanafanya hivyo ili kulinda nafasi zao lakini wakimng'ong'a kwa wanachokifanya, ambacho hakisaidii mpaka anawambia watumie mtindo wa Mwenezi wa CCM kusikiliza wananchi.

Inashangaza pia unaweza kumsikia msaidizi mwingine wa Rais akizungumzia eneo lake kwa kulalamikia walio chini yake, badala ya kuwachukulia hatua akithibitisha kuwa wanaharibu lakini akichelea kugusa wateule wenziwe.

Inatokea hivyo ingawa Rais alishawaambia fanyeni na hata kama mtakosea tutajua lakini hatua iwe imechukuliwa inayosaidia wananchi kuondokana na kero na kadhia za kimaendeleo.


Ila sababu za kuhamisha baadhi ya wateule ziliniacha hoi kwamba wewe nimekuondoa hapo kwa sababu hukuwa unaendana na wa huko na wewe nakupeleka pale kwa asababu utaendana na wa huko, kwani aliyekutangulia alikuwa nyapara, akitumia mabavu.

Mama, Watanzania ukiwapeleka kwa mbeleko watakukojolea mgongoni na kukuchania mbeleko, mtu akiharibu mahali apumzishwe, si kumweka pembeni na kumrudisha eti kajirekebisha wakati una Watanzania zaidi ya milioni 60 na wote ni wako, na baadhi yao ni wasomi wenye uwezo stahiki wa nafasi hizo.

Kazi Iendelee!

# Samia na dhamira ya kuondoa giza mijini, vijijini

**Na Mwandishi Wetu**



Mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP)

MIAKA mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, madarakani, imechochea utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya umeme ambayo inalenga kuiondoa Tanzania gizani na kuwa na mipango ya kuuza nishati hiyo nje ya nchi.

Mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP), unaolenga kuzalisha megawatt 2115, tayari umeanza kazi na kupunguza mgawo wa umeme kwa asilimia 85. Hii ni baada ya mwezi uliopita, serikali kuingiza megawati 235 kwenye gridi ya Taifa baada ya kuwasha mtambo namba tisa.

Kama hiyo haitoshi, baadaye mwezi huu, Rais Samia na Rais wa Misri, Abdel-Fatah Alsisi, watazindua mtambo namba nane na hivyo kuwezesha nchi kuwa na megawati za nyongeza kwenye gridi ya taifa kuwa 470.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko, alisema kwa sasa upatikanaji wa umeme ni asilimia 98 na kwamba mgawo umepungua na utakwisha siku za karibuni.

Taarifa zinaonesha kwamba Rais Samia alipoingia madarakani mwaka 2021, aliukuta mradi huo ukiwa asilimia 33 ya utekelezaji tangu ulipoanza kujengwa mwaka 2015.

"Amehakikisha fedha zinapatikana na kulipwa kwa wakati kwa mkandarasi ninafurahi kusema kile nilichokuwa nimeahidi kwamba Februari 25, mtambo namba tisa unaingiza megawati 235 kimetimia. Hii ni kutokana na msukumo mkubwa.

Kwa ratiba tuliyokuwa nayo ya kawaida umeme huu ungefikia mwezi wa sita ila kwa msukumo mkubwa wa Rais Samia tumefanikisha," alisema Biteko.

Kabla ya kuwashwa kwa mtambo huo, nchi ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa megawati 200 hadi 400 na kwamba matarajio ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuondoa mgawo mwishoni mwa mwezi huu.

"Nafurahi kuwaambia Watanzania uwekezaji umejibu, tumepata umeme pamoja na siasa nyingi na magumu tuliyopitia jambo muhimu Watanzania wanataka umeme hawataki maneno, tumechagua kutenda zaidi kuliko kusema," alisema.

Kwa mujibu wa Biteko, mahitaji ya umeme yanaongezeka na kwamba serikali imeongeza vyanzo vingine ili kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana.

Wachambuzi wanaeleza kuwa uwekezaji mkubwa unaoonekana kwenye sekta ya nishati ni kutokana na ndoto ya serikali kujenga uchumi wa viwanda.

Mathalani, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia, Mkoa wa Pwani, umeshuhudia ongezeko la viwanda na kwamba hivi sasa 17 viko katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji.

Mwezi uliopita, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alikaririwa akisema kuna viwanda 1,533 vikubwa, 120 vya kati na 124 vidogo ambavyo vinahitaji umeme wa uhakika.

Mradi wa JNHPP una thamani ya Sh. trilioni sita ukitegemewa kuzalisha megawati 2,115 za umeme utakapokamilika.

Mradi wa JNHPP unashika nafasi ya kwanza kwa ukubwa katika miradi yote inayotekelezwa katika nchi za Afrika Mashariki na ni wa nne kwa miradi yote inayotekelezwa Afrika.

Mradi unaoshika nafasi ya kwanza Afrika ni wa Grand Ethiopian Renaissance Dam (6,400 MW) ulioko nchini Ethiopia, namba mbili ni ule wa Batoka George Hydroelectric Dam (2,400 MW) wa Zambia katika Mto Zambezi na wa tatu ni mradi wa Caculo Cabaco Hydroelectric Dam (2,172 Mw) wa Angola.

Agosti, mwaka jana, kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme cha Ifakara (Ifakara substation), kilikamilika na hivyo kuzihakikishia umeme wa uhakika wilaya za Kilombero na Ulanga, mkoani Morogoro na hivyo kuondokana na adha ya kukatika kwa umeme.

### NYAKANAZI-KIGOMA, UMEME JUA

Katika kipindi cha miaka mitatu, mkoa wa Kigoma umepata unafuu na uhakika wa umeme kutoka utegemezi wa nishati hiyo kutokana na kufuliwa na majenereta hadi umeme jua na sasa wa maji kutoka mto Malagarasi.

Tayari mradi wa jua wa megawati tano umekamilika na kuziondoa zaidi ya kaya 65,000 gizani.

Mwezi uliopita, serikali ilisaini mkataba wa kuzalisha megawati 49.5 kwa nguvu ya maji katika mto Malagarasi, mkaoni humo. Waziri Dk. Biteko alishuhudia tukio la kusaini mkataba huo ambao utagharimu dola za Marekani milioni 144.14 na utajengwa ndani ya miezi 42.

Dk. Biteko alisema mbali ya mradi wa Malagarasi, mkoa wa Kigoma una miradi mingine mitatu ukiwamo wa ujenzi wa njia ya usafirishaji wa umeme kutoka Nyakanazi hadi Kigoma (KV 400), Tabora hadi Kigoma (KV 132) na kuongeza uwezo wa kituo cha umeme jua kutoka megawati tano hadi 10.

Kwa mujibu wa Dk. Biteko, serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya umeme nchi nzima ikiwamo ujenzi wa vituo 24 vya kupoza umeme katika maeneo ya kimkakati ili kuimarisha gridi ya taifa.

### TAZA RUKWA

Mapema mwaka huu, serikali ilieleza kupeleka umeme wa gridi mkoani Rukwa kupitia mradi wa TAZA, ulioanza kutekelezwa Novemba, 2023 unatarajiwa kukamilika Agosti, 2026, ikiwa ni jitihada za kuhakikisha maeneo yote nchini yanapata umeme wa uhakika.

### RUSUMO

Huu ni mradi wa kuzalisha megawati 80 za umeme na unatekelezwa kwa pamoja na nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi ambazo zimeanza kupata nishati hiyo kutoka kwenye mradi huo.

Desemba, mwaka jana, mawaziri wa nishati kutoka nchi hizo waliridhishwa na utekelezaji wake na wakakubaliana kwamba uzinduliwe mradi huu na kumtaka mkandarasi kukamilisha mradi huo mapema na atoe cheti cha kukamilisha mradi.

Mradi wa umeme wa Rusumo utazalisha megawati 80 ambapo kila nchi itapata megawati 27.

### MIKATABA 14 UMEME VIJIJINI

Februari 14, mwaka jana, Rais Samia alishuhudia tukio la kihistoria la utiaji saini mikataba ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini pamoja na uimarishaji gridi ya taifa.

Mikataba 14 imetiwa saini baina ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kampuni mbalimbali ikihusisha miradi mitatu mikubwa ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 1,522 katika mikoa tisa, maeneo 336 ya wachimbaji wadogo wa madini na vituo vya afya, pampu za maji 399 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 108,178.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa upande wake, limetia saini mikataba sita kwa ajili ya miradi 26 ya kuimarisha gridi ya Taifa.

Katika tukio hilo lililofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Samia alisema miradi hiyo inalenga kuwanufaisha wananchi kwa kushamirisha uchumi na biashara kwa ajili ya kuinua hali zao za maisha.

### KUIMARISHA GRIDI

Mikataba sita ya kuimarisha iliyosainiwa mwaka jana ililenga kujenga mradi mkubwa wa umeme wa kuimarisha Gridi ya Taifa ambao utaigharimu serikali Sh. trilioni 4.42 ambao utakamilika ndani ya kipindi cha miaka minne.

Kukamilika kwa mradi huo itakuwa ni historia kubwa kwa nchi kwa kuwa kutawahakikishia wananchi uhakika wa umeme na lengo la serikali ni kufikisha megawati 5,000 za umeme kwenye vijiji vyote ifikapo 2025.

Hadi Januari, mwaka jana, huduma ya umeme ilikuwa imefika katika vijiji 9,467 kati ya 12,345 Tanzania Bara sawa na asilimia 76.7.

Kwa upande wa vitongoji, kati ya 64,760 vilivyopo nchini, 28,424 sawa na asilimia 43.9 vilikwishafikiwa na huduma ya umeme. Serikali inaendelea na mipango ya kuongeza mafungu katika Mfuko wa Nishati Vijijini ili kuongeza kasi ya kufikisha umeme katika vitongoji 36,336 vilivyobaki.

Upatikanaji wa umeme wa uhakika unachangia ukuaji wa uchumi katika maeneo ya vijijini, kuboresha huduma za jamii vijijini zikiwemo afya, elimu, maji safi, mawasiliano na usalama pamoja na kuhifadhi mazingira na kuimarisha usalama.

Wachambuzi wa masuala ya maendeleo wanaeleza hatua ya kuzalisha umeme na kuusambaza kwa wananchi, itatengeneza ajira nyingi za moja kwa moja na zisizo rasmi hususani vijijini na hivyo kupunguza uhamiaji mijini kwa vijana.


MAISHA
MACHI 17, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili


# PICHICHI TURBAN-2
# Mbunifu anayethaminiwa Tanzania






## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | R | U | N | G | U |
| A | | | | Y | | N |
| J | | D | A | U | | G |
| E | D | A | | K | U | U |
| S | | I | N | A | | Z |
| H | | M | | | | W |
| I | G | A | N | A | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

FAA,NOA, RAI, IBA, IDAKE, TAIFA, FANYA, IMARA, ANDIKIA, USHINDI

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Watoto wawili walikuwa wakigombea mapera, mama mmoja alitokea na kuwaamulia na kuwataka kila mmoja kusema tatizo ambalo limewafanya kugombana.

Juma: John ndiye mgomvi alinipora mapera yangu

John: Hapana yeye ndiye mgomvi alichukua mapera katika mti aliopanda baba

Juma: Ule mti umejiotea pale msituni, huyu ni muongo

Mama: Nyinyi wote nawaona mnadanganya ugomvi haufai kwa sababu huleta chuki

John: Kweli mama hata mwalimu alisema heri nusu shari, kuliko shari kamili

SWALI

Je sukari inayotumika nyumbani inatengenezwa kutokana na zao gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mke anapokuwa mlevi kupindukia akipinga uke wenza!

KARIBU msomaji tuendelee na vituko ndani ya familia zetu. Migongano ya wanandoa katika ndoa imezua mitafaruku mingi. Wengine wanadai talaka, wengine wanaondoka, wengine wanadai mgawanyo wa mali.

Yuko anayedai urithi mapema ili huko mbele ya safari asije akaambulia patupu. Na hii ni baada ya mumewe kung'ang'ania kuoa mke mwingine na mkewe kutoa masharti ya kupewa mali ili aruhusu uke wenza.

Kabla sijasimulia kisanga kingine kinachohusu uke wenza wa kulazimisha, hebu tusikie mchango wa maoni toka kwa msomaji wetu kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani kuhusu mada ya wiki iliyopita.

Anasema: "Tatizo lipo pande zote, japo kwa wanaume ni zaidi. Hii inatokana na misingi mibaya inayoanzia kwenye malezi hadi ukubwani. Namwomba mama huyo awe mtulivu, alee watoto wake na hii ndiyo tafsiri ya maisha. Asisumbuke na mali za baba huyo, aendelee kufanya kazi kwa bidii na kuomba Mungu atampatia hitaji. Vile atoavyo kwa wanaume pia hutoa kwa wanawake kwani sote Mungu alitubariki. (Msomaji Dar).

Naam. Yuko msomaji mzuri wa safu hii ambaye ni mwanamama alinipigia simu baada ya kuisoma makala ya wiki iliyopita, kisha akanisimulia kisa cha mama mmoja ambaye hivi sasa ameamua kuwa mlevi kupita kiasi, kisa mumewe kahamia kwa mdada mmoja ambaye anataka kufunga naye ndoa.

Kwa mujibu wa maelezo ya mama huyu aliyenimegea kituko hicho, wanawake hawa walikuwa wanakutana mara kwa mara sehemu za burudani lakini walikuwa hawajuani.

Kila bwana huyo anapomtoa outing mkewe, pia alikuwa akimwambia girlfriend wake anayetaka kumuoa aje sehemu hiyo japo walikuwa hawakai meza moja.

Ikawa ni mazoea wanawake hawa wakionana sehemu hizo za burudani kama bwana hajafika, walikaa meza moja. Na hata bwana akifika, bibie (girfried) akitaka kuondoka, yule mama alimwambia akae tu.

Kumbe ni kimada cha mumewe yeye hajui akidhani ni rafiki tu. Ule ulikuwa ni moshi unaofuka, lakini sasa moto umewaka kabisa.

Bwana japokuwa alikuwa hajafunga ndoa na mkewe, lakini wamezaa watoto wawili. Penzi la nje sasa limekolea, jamaa yuko full na bibie na mama watoto amegundua kwani hata mumewe amebadilika, jeuri na anaweza kupitiliza wiki bila kurudi nyumbani.

Baada ya bi-mkubwa kuchunguza akagundua kuwa kumbe ni mwanadada waliyekuwa wakikutana ndiye msaliti wa penzi lake. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mambo yakawa hadharani. Bimkubwa ilifikia hatua akapata simu ya mdada huyo na kumpigia akimlalamikia kuhusu kumpora mumewe, lakini majibu aliyopata yalimkasha tamaa.

Mdada huyu akawa anamwambia mke mwenza aende kwenye mazoezi apunguze unene kama anataka mumewe amrejee kwani anataka 'vipotabo' yaani wembamba.

'Jambo hili ndilo limemfanya bi-mkubwa achanganyikiwe na kuanza kunywa pombe mfululizo. Na zaidi pia ni kutokana na fununu kuwa huenda bwana huyo akafunga ndoa na bibie huyo hivi karibuni'.

Uke wenza bado ni tatizo linalobomoa baadhi ya familia zetu. Lakini wapo kinamama inaonekana kukubaliana na hali hiyo kuepusha shari. Nini kinatokea?

Tayari tumemsikia mama aliyedai urithi mapema kabla ya kukubali uke wenza, mwingine mlevi baada ya kusikia mumewe anakusudia kuoa mwanadada waliyekuwa wakivinjari wote kwenye burudani.

Mama huyo aliyeamua kuwa mlevi anayo haki ya kutetea nafasi yake kama mke halali. Binafsi ningemshauri maadam yuko nyumbani kwake na hajafukuzwa, awe mpole. Isitoshe ana kazi yake nzuri ajikite kwenye kazi ili kuhakikisha anatunza watoto wake! Mume huyo bado anao wajibu wa kumtunza na watoto, endapo hafanyi hivyo zipo hatua za kuchukua kisheria.

Na zaidi, yule bwana kachepuka tu. Si ajabu hata huko anakofikiria kuwa ni sabuni ya roho kukamchachia akarejea kwenye boma lake kwa msamaha.

Hata hivyo, lipo jambo moja nimekuwa najiuliza na limejitokeza katika matukio niliyozungumzia hapo juu; kwamba kwa nini mwanaume anapotaka kuthibitisha mahusiano yake nje ya ndoa humuunganisha kwa simu mkewe na mwanamke huyo wa nje? Unadhani njia hii ni sahihi?

Na hili la baadhi ya kinababa kutelekeza nyumba zao na kuanzisha nyumba nyingine kibabe bila kupata ridhaa ya mkewe, unaweza kulizungumziaje msomaji wangu?

**Je, una maoni, ushauri? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Tukimbilie kuanzisha WMA au kambi za uwindaji?

JUMUIYA ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA), ni eneo kwenye ardhi ya kijiji au vijiji iliyokubalika na kutengwa kwa misingi ya kuhifadhi wanyamapori na kwa ajili ya biashara inayotokana na uhifadhi huo katika taifa letu.

Usimamizi wa shughuli za jumuiya hizi, kisheria unaratibiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Katika maeneo yanayopakana na hifadhi za taifa, serikali imeruhusu jamii kuanzisha hifadhi za wanyamapori, hususan kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi za taifa au hifadhi nyingine.

Ruhusa hiyo pia inatoa fursa ya kuanzishwa jumuiya hizo kwenye ushoroba (njia maalum za wanyama), ambapo wanyama wanasafiri kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta chakula, maji na mahitaji mengineyo.

Ni muhimu kukumbuka kuwa WMA si hifadhi ya taifa na wala si mwendelezo wa hifadhi za taifa au ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi, isipokuwa vijiji vinaweza kutoa leseni kwa wawekezaji binafsi ili kujenga miundombinu, ama kuendesha shughuli zao ndani ya maeneo ya WMA, mfano kujenga kambi na kuendesha uwindaji.

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 inabainisha kuwa jamii itakuwa na mamlaka yote ya kusimamia na kupata manufaa kutokana na juhudi zao za uhifadhi ingawa umiliki wa rasilimali za wanyamapori unabaki kwa serikali.

Hata hivyo, Kanuni za WMA za Mwaka 2018 zinaeleza kuwa mgawanyo wa manufaa utaelezwa 'na waraka utakaokuwa ukitolewa mara kwa mara', ambao ni waraka wa mwaka 2020,

Waraka huo pamoja na mambo mengine, unaeleza kuwa mapato yatokanayo na shughuli za uhifadhi yaende moja kwa moja kwa Serikali, ambayo itarudisha sehemu ya mapato hayo kwenye WMAs.

Kwenye chanzo cha mapato ambayo ni ada ya kitalu, TAWA inanufaika na asilimia 25, WMA asilimia 75, wakati katika ada ya uwindaji, TAWA inachukua asilimia 25, WMA asilimia 55, halmashauri husika inanufaika kwa asilimia 10 na asilimia 10 inakwenda Hazina (Mfuko Mkuu wa Serikali).

Aidha katika ada ya uhifadhi, TAWA inapata asilimia 25, WMA inachota asilimia 45, Halmashauri inaambulia asilimia tano na Hazina asilimia 25.

Vilevile, suala la ada ya watazamaji TAWA inanufaika kwa kupata asilimia 25, WMA asilimia 60, Halmashauri ya Wilaya asilimia tano na Hazina, asilimia 10.

Wakati ada inayotokana na kibali, TAWA inapata asilimia 25, WMA inanufaika asilimia 30, Halmashauri inapata asilimia tano na Hazina inachukua asilimia 40.

WMA zinafanya kazi kubwa katika uhifadhi kwa kudhibiti ujangili wa wanyamapori na kutatua mwingiliano wa binadamu na wanyama wakali na waharibifu.

Ni kweli Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea na juhudi za kuhakikisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi, wananufaika na rasilimali zilizopo.

Kupitia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori, jamii zinanufaika kwa kupata ajira, kitoweo, elimu, miradi ya kijamii na kuongeza kipato.

Aidha, wananchi wanaoishi jirani na misitu wananufaika kupitia miradi ya ufugaji nyuki ambapo kupitia uwezeshaji wa Mfuko wa Misitu Tanzania,

Iko miradi mingi imeanzishwa kwa ajili ya kuboresha kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu imetekelezwa.

Faida nyingine ni udhibiti wa migogoro baina ya wananchi na hifadhi. Katika kudhibiti migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo jirani na hifadhi, jumuiya nyingi za uhifadhi za kijamii zimeanzishwa.

> **"Ni kweli Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea na juhudi za kuhakikisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi, wananufaika na rasilimali zilizopo.**

WMA hapa nchini zinachukuliwa kama ni kinga (buffer) muhimu kwa maeneo ya hifadhi za taifa, mapori ya akiba, Hifadhi ya Ngorongoro na mapori tengefu.

Kutokana na faida na umuhimu wake kiuchumi kwa jamii zinazozunguka maeneo yanayoruhusu jamii kunufaika na fursa hiyo, ni vyema wadau wa uhifadhi nchini wakaendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuendeleza WMA ili kuziwezesha kujisimamia na kujiendesha.


Pamoja na hayo, kupitia ushirikishwaji huo, jamii zitakuwa zikinufaika na matunda yatokanayo na shughuli za uhifadhi katika maeneo yao kwa kujiletea maendeleo na huduma za kijamii ikiwamo shule na zahanati.

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# Send-off



Ni kumbukumbu isiyosahaulika kwa familia ya Lucy Mwaitete baada ya Juni 18, mwaka jana kumfanyia sherehe ya kipekee ya kumuaga binti yao katika ukumbi wa JC Mbezi Beach Dar es Salaam. Ndoa yake na Moses Osani, ilifanyika Julai 2, mwaka jana katika Kanisa la Wasabato la New Life jijini Nairobi nchini Kenya







# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# PICHICHI TURBAN-2

## ‘Mbunifu anayethaminiwa Tanzania

UMAARUFU wa mavazi ya Stara umeongezeka nchini na hata duniani kote, hivyo kuwafanya wabunifu kama Pichichi kufikiria nje ya boksi.

Hapa nchini umaarufu wa vazi hili umetokana na harakati nyingi yakiwemo majukwaa kama Stara Fashion Week. ambalo hufanyika kila mwaka .

Katika wabunifu wanaomuangalia kwa jicho la karibu, Said Ndee maarufu Pichichi Turban ambaye amebuni vazi la ‘Juba la Ramadhan’

Katika sehemu ya pili ya simulizi yake tunaangalia namna alivyojikita katika ubunifu wa mitindo kibiashara.

**Kujiingiza kibiashara**

Mwaka 2020 aliamua kijiingiza katika biashara rasmi baada ya kuona inamlipa kwa kuanza kufungua mtandao wa kijamii kwa jina la PichichiTurbans, huko akaanza kusambaza vilemba vyake na kufanya watu wengi waanze kuvutiwa naye.

Anasema kupitia mitandao ya kijamii alianza kupata wateja mbalimbali, lakini changamoto ikawa wateja wapotaka kupafahamu ofisini kwake wakati hakuwa na ofisi. “Watu wengi walikuwa wakijua Pichichi ni mwanamke kutokana na picha nyingi za kazi zangu kuonekana wanawake, watu wakawa wananiuliza dada tunakupata wapi. Jambo hilo lilikuwa linanifanya mpaka nashindwa kujitokeza mimi kama mimi,” anasema.

Anasema Julai 2020 alienda kupeleka bidhaa zake kwenye maonesho ya biashara ya kimataifa maarufu kama Sabasaba yaliyokuwa yakifanyika mkoani Dar es Salaam na ndipo akapata mwangaza mkubwa baada ya watu kuzidi kutamani kujua ofisi yake ilikuwa wapi.

Kwa mujibu wa Ndee, alimpa dada mmoja aliyejulikana kama Christina, raia wa Kenya bidhaa zake na dada huyo akamfundisha jinsi ya kutanua biashara yake kwa njia nyingine zaidi.

Anasema alianza kushona vilemba kofia vya aina tofauti tofauti na kupita Kariakoo kwa watu wenye meza na kuzisambaza ili wauze.

Kofia zinazobaki alikuwa akizipitia jioni na faida inayopatikana wakawa wanagawana na hapo akatengeneza mtandao mkubwa wa wafanyabiashara wadogo wenye meza kwa ajili ya kumuuzia biadhaa zake hizo.

“Sasa kitu cha msingi kilikuwa ni wapi kupata ofisi, maana Kariakoo gharama ilikuwa kubwa sana. Hivyo ikabidi nipambane sana,” anasema.

**Vazi la stara**

Anasema mwaka 2021 alipata fremu maeneo ya Kariakoo karibu na Hoteli ya Wanyama na aliamua kununua cherehani mbili, kwa hiyo upande mmoja aliweka cherehani kwa ajili ya kushona na upande wa pili akaigeuza eneo la kuuzia kofia zake.

Saidi anasema duka hilo likawa ndiyo sehemu yake na wateja wake wote akawa anawaonesha, hata wafanyabiashara wadogo wadogo wakawa wanamfuata na siyo tena kuwapelekea mizigo.

Anasema tayari akili yake ikazama ni jinsi gani anaweza kutengeneza fedha zaidi, aliamini biashara ya kofia inaenda ipo siku itabadilika na huenda soko likapotea kabisa.

Anaongeza kuwa akafikiria kubuni vazi ambalo litaendana na kofia hizo, kwa kuwa hata wateja wake nao walipokuwa wakiagiza kofia kupitia mtandaoni walikuwa wakiuliza na mavazi watayapata wapi.

Saidi anasema kama ilivyokuwa kwa kofia aliweza kupambana na kubuni vazi lake la kwanza, ambalo aliliita jina la ‘Hijabu ya kisasa’ ambalo aliliingiza sokoni mwaka 2021 na lilifanya vizuri zaidi.

Itaendelea Jumapili

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# HEWA SAFI

TATIZO la kunuka kinywa humfanya mtu apate msongo wa mawazo,pia huharibu uhusiano kati ya wenza, ndugu, jamaa na marafiki.

Bahati mbaya Watanzania wengi wenye tatizo la kunuka mdomo hawajitambui mpaka aambiwe na watu wengine wa karibu tena wenye upendo.

Kwa bahati mbaya tatizo la kunuka mdomo humuondolea mwanamke uwezo wake wa kujiamini na kujiona siyo mrembo katikati ya wanawake wenzake.

Kuna njia kadhaa za kutumia kumaliza tatizo hili na ni muhimu kukizifuata.

**SAFISHA ULIMI VIZURI**

Watu wachache sana huchukua zaidi ya nusu kusafisha ulimi kutokana na ulimi unatunza sana uchafu katika kinywa.

Hata hivyo, njia rahisi tumia kijiko kutoa uchafu au nunua kifaa cha kusafisha ulimi kwa bei nafuu katika maduka ya dawa ili kujisafisha.

**KISAFISHA MIDOMO**

Njia nyingine rahisi ya kupata harufu nzuri tumia maji ya chumvi kusuuza mdomo wako.

Tumia kisafisha midomo ambacho hakina gharama kununua na hakina madhara.

Weka chumvi kwenye glasi ya maji na sukutua

**MDALASINI NA HILIKI**

Hivi viungo vinatumika toka kale kuweka harufu nzuri mdomoni.


Ukila vyakula vyenye viungo vingi au ukihisi mdomo haueleweki chukua punje ya hiliki au kipande cha mdalasini tafuna.

Ukiweza chemsha maji ya viungo hivi na sukutua.

**TUFAA, TANGO**

Matunda haya yanaongeza mate mdomoni na kuzuia uwepo wa bakteria ambao husababisha harufu mbaya. Kula kipande cha tango au tufaa (apple) hasa baada ya chakula. Pera husaidia wale wanaotoka damu kwenye fizi pia.





## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Juisi ya maganda ya nanasi



MAGANDA ya nanasi yanaweza kutoa juisi ama sharubati tamu zaidi sawa kabisa na tunda lenyewe.

Juisi hii inafaa sana kutengeneza hata kama hakuna umeme.

**Mahitaji**

Maganda ya nanasi, tangawizi, maji, sukari na vipande viwili vya limao.

**Maandalizi**

Osha maganda ya nanasi na tangawizi kwa maji safi kisha katakata na uweke kwenye sufuria tayari kwa kuchemsha.

Washa jiko, bandika sufuria yenye maganda ya nanasi na tangawizi. Weka maji kiasi chako kwenye sufuria yako kisha ufunike uache ichemke kwa dakika 30 hadi maji yatakapobadilika na kuwa na rangi ya njano.

Maandalizi ya juisi hii ni rahisi haitumiki blenda inayotumika wakati wa kusaga aina nyingine za juisi, hivyo hata kama umeme umekatika bado unaweza kutengeneza juisi hii na kufurahia pamoja na uwapendao.

Ongeza maji ya limao au ndimu na vipande vya barafu, mpaka hapo juisi yako ipo tayari kwa kunywa. Iwapo hupendi barafu, endelea kufurahia ikiwa ya moto.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Usafi wa nyumba nao una mpangilio wake

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

Mwingine anaweza kusema mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka, lakini ninachotaka kueleza ni kwamba ni namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuiimarisha na ikadumu zaidi kama ambavyo ni kinyume kwamba isiposafishwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.

Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba, hakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.

Kwenye maeneo yote ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiliwa,



hakikisha unafanya hivyo, kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Pia baada ya kusafisha hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha kwamba yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndio utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.

## DONDOO

# Unajua viungo ni pambo?

**Na Restuta James**

Iliki, mdalasini, tangawizi iliyokaushwa, mchaichai, karafuu, karanga na mahindi ya bisi ni pambo zuri, kama likipangiliwa vyema.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Esther Donald, anasema ili kutumia pambo la aina hiyo, unapaswa kuwa na jagi maalumu la kioo au linaloangaza.

Anasema unachopaswa kufanya ni kuweka tangawizi iliyokaushwa kiasi, karafuu na iliki.

"Inategemea na ukubwa wa chombo chako cha kupambia, unaweza kuweka nusu kikombe cha chai cha kila kiungo. Kila kimoja kinapaswa kuonekana kwa hivyo usivikoroge," anasema.


Esther anasema pambo la viungo linaweza kuwekwa kwenye stendi eneo la chakula (dining) au sebuleni ambako mchanganyiko unaweza kuwa wa karanga na korosho.

Hata hivyo, anashauri kwamba pambo la viungo linaweza kuboreshwa kwa kuwekewa jagi lingine lenye maua kama inavyoonekana pichani.

Tuwasiliane kupitia restuta-james@gmail.com au 0753333330
.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... SIO MAISHA TU HATA SIKIO UNATOBOA....

MAKALA

# Mfuko wa SELF kimbilio mikopo nafuu wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Msajili wa Hazina imeweka utaratibu wa taasisi zilizo za serikali kufanya vikao kazi na wahariri na wakuu wa vyombo vya habari kuelezea mafanikio, changamoto na mikakati katika kuleta maendeleo ya kisekta na kuchangia pato la taifa kwa ujumla.

Machi 11, mwaka huu, ilikuwa zamu ya Mfuko wa SELF (SELF Microfinance Fund), ambao ulifichua mambo ambayo yalikuwa yamejificha nyuma ya pazia kuhusu mchango wake na mikakati ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo ili kuwawezesha kupata huduma za kifedha kwa ajili ya kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Kwa kawaida, ili kupata mkopo katika benki kwa wajasiriamali kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza biashara imekuwa sawa na mfupa uliomshinda fisi. Lakini SELF imeonyesha hilo linawezekana kupitia mfuko huo katika kuwawezesha wajasiriamali huku kukiwa na shuhuda ambazo zimebainisha wajasiriamali walivyonufaika na mikopo hiyo bila masharti magumu yanayoweza kuwakatisha tamaa.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo, Mkurugenzi wa maendeleo ya Biashara wa SELF, Petro Mataba, anasema mfuko umekuwa mkombozi na kimbilio la wajasiriamali wadogo na wakati kwa kuwakopesha mabilioni ya shilingi na matunda yake yameonekana.

Mataba alisema hadi kufikia Desemba 31, 2023 walikuwa wametoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 324.51 ikiwa na kiwango cha mikopo chechefu chini ya asilimia 10 na kujiendesha kwa faida. Mikopo hiyo, iliwafikia wanufaika 314,000 wakiwamo wanawake 166,000 na wanaume 147,000 kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.



Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa SELF, Petro Mataba.

Licha ya kuwakopesha watu hao mabilioni hayo ya fedha, Mataba alibainisha kuwa kupitia matawi yake 12 yaliyoko katika mikoa mbalimbali nchini, pia taasisi 200 zinanufaika na mikopo inayotolewa na taasisi hiyo.

"Mfuko umetengeneza ajira 37,000 kutokana na wanufaika wanaochukua mikopo sanjari na kutoa elimu ya fedha kwa wanufaika 1517," alisema Mataba na kubainisha kuwa mikopo hiyo imechangia upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati.

**RIBA ZA MIKOPO**

Kilio kikubwa cha wananchi kwa muda mrefu ni riba za mikopo zinazotolewa na taasisi za fedha hususan benki za biashara pamoja na masharti yanayowafanya wengi kushindwa kupata huduma hiyo. Viwango vya riba katika benki ni kati ya asilimia 20 na 25.

Mfuko wa SELF katika kutatua changamoto hiyo umeweka masharti nafuu na viwango vidogo vya riba kulinganisha na taasisi kubwa za kifedha.

Katika mikopo kwa taasisi ndogo za fedha (MFI) na vyama vya akiba vya kuweka na kukopa (SACCOS) kwa wale wanufaika wanaofanya biashara au kilimo, riba ni kati ya asilimia 16 na 18 kwa mwaka.

Kwa mikopo ya moja kwa moja kwa wanufaika ambayo walengwa wake ni wajasiriamali wadogo na wakati (MSME), wakulima wadogo na wafugaji, mikopo kwa ajili ya kuboresha makazi, vikundi, mikopo ya nishati safi ya kupikia na watumishi wa umma, riba yake ni ya asilimia 15 na 22.

**ILIKOTOKA**

Akizungumzia historia ya mfuko huo, Mataba alisema ulianza kutekeleza majukumu yake Julai Mosi, 2015 ukiwa ni taasisi ya serikali chini ya Wizara ya Fedha na sasa ni moja ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Lengo la mfuko huo ni kutoa mikopo kwa wananchi wa kipato cha chini kuwawezesha kujishughulisha na uzalishaji mali ili kujiongezea kipato na kupunguza umaskini.

"Majukumu makubwa SELF ni kutoa huduma za mikopo midogo kwa watu binafsi, vikundi, na taasisi ndogo za fedha zinazolengwa na serikali, ili kulea na kukuza sekta ya huduma ndogo za fedha kwa ajili ya kupunguza umaskini.

"Nyingine ni kutambua, kuendeleza na kukuza fursa za kuwezesha ajira kwa wajasiriamali wadogo kwa kuwapa mikopo, elimu ya utendaji kazi, na mafunzo kwa ajili ya kuboresha stadi zao. Pia kuandaa na kuweka utaratibu na mikakati ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo, ili kuwawezesha kupata huduma za kifedha kwa ajili ya kujiajiri kwa tija," alisema.

Katika kutekeleza hayo, alisema Mfuko wa SELF hutoa mikopo kupitia taasisi ndogo za fedha ili kusaidia kupeleka huduma za kifedha ambako haufiki pamoja na mikopo ya moja kwa moja kwa wanufaika.

"Sambamba na hilo, elimu ya fedha na kuzijengea uwezo taasisi ndogo za fedha na hii hutolewa na wajasiriamali wote. Wateja wa vikundi hupewa mafunzo kuhusu vikundi na taasisi za huduma ndogo za fedha hupewa mafunzo ya kujengewa uwezo wa kuendesha taasisi zao," alisema.

**USHUHUDA MZITO**

Uko ushuhuda katika matokeo ya huduma za mfuko kutoka kwa wanufaika wakiwamo wa sekta za viwanda na elimu. Wanufaika hao wamepiga hatua katika shughuli zao baada ya kupata mikopo iliyowawezesha kuzipaisha kampuni na taasisi zao.

Kampuni ya Star Natural Product Ltd ambayo iko katika sekta ya viwanda vidogo vidogo. Ilianza kukopa ikiwa na mtaji mdogo na mpaka sasa imejiendeleza na kufikia mkopo mkubwa. Kutokana na uwezeshaji huo, kampuni imekuza karakana ya kutengeneza mafuta na sabuni kutokana na mchikichi.

Kutokana na maendeleo hayo, kampuni imepanua wigo wa biashara kwa kufungua vituo viwili vya kuchakata mafuta ya mchikichi, Mkuranga na Kibiti. Vituo hivyo vimesaidia wakulima 300 katika maeneo hayo kupata huduma ya kukamua mafuta.

Bright Future Academy ya Zanzibar mnufaika mwingine wa huduma za Mfuko wa SELF. Taasisi hiyo ilianza kukopa ikiwa na mtaji mdogo lakini kutokana na uwezeshaji toka SELF imetoka kupanga nyumba ya vyumba vinne vya madarasa na kununua kiwanja na kujenga shule yenye madarasa 32 na kuendelea kujipanua zaidi.

Taasisi hiyo imenufaika kwa kukopa mara tatu kwenye mfuko huo. Ilianza kukopa SELF kipindi ambacho haikuwa na sifa ya kukopesheka kwenye taasisi zingine za fedha mpaka kufikia uwezo wa kukopa zaidi ya milioni 300.

Awali, shule hiyo ilikuwa na wanafunzi 300 na sasa wamefikia wanafunzi 1,470. Kutokana na mazingira mazuri ya kusoma, imefanikiwa kuwa shule ya kwanza Zanzibar kwa kufaulisha kwa miaka miwili katika matokeo ya darasa la saba.

**ELIMU YA FEDHA**

Katika safari yoyote kuna milima na mabonde. Ndivyo ambavyo SELF imekumbana na changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ikiwamo wananchi wengi kutokuwa na elimu ya fedha.

Hali hiyo imesababisha wananchi wengi hasa wa kipato cha chini kukosa uelewa wa kutosha wakati wa kufanya uamuzi wa kukopa fedha au kutumia mikopo nje ya malengo yaliyokusudiwa. Aidha, wananchi wengi bado hawana utamaduni wa kurejesha mikopo kwa hiari.

Sambamba na hiyo, kuna changamoto ya wananchi wengi wa kipato cha chini kujishughulisha na biashara zisizo rasmi mfano Machinga. Hii inasababisha wengi kushindwa kukopesheka kutokana na kuwa katika mfumo usio rasmi.

Kutokana na kuwapo kwa changamoto hizo, Mataba alisema mfuko umejiwekea mkakti wa kuwafikia wateja wengi zaidi hasa wa kipato cha chini na kwamba hilo litawezekana kwa kuongeza utoaji wa mikopo,kusogeza huduma karibu na wananchi na kuwafikia walengwa wengi zaidi.



Mjasiriamali wa mboga na nyanya.



Wajasiriamali wa viungo.

MAKALA

# SIFA HUPOFUSHA JAMII, UKOSOAJI HUFUMBUA JAPO UNAWEZA KUPUUZA



Na Magabilo Masambu

**Kilichonisaidia ni kukubali kwamba sikuwa najua kila kitu. Leo wale waliokuwa wakinikosoa ndio wanaonipongeza na ninawashukuru sana pengine wasingefanya hivyo leo nisingikuwa mwandishi mzuri kama wanavyosema wenyewe leo.**

ZAMANI nilipokuwa mdogo nilikuwa nashangaa sana. Bahati nzuri niliishi na babu yangu nikiwa mdogo. Kuna jambo nilikuwa silielewi lakini sasa nimekuwa mtu mzima nina familia ndiyo nimeelewa kwa nini ilikuwa vile.

Lilikuwa jambo la kawaida babu yangu kutoshinda nyumbani mara nyingi, nikawa najiuliza mbona hii tabia ina wazee wengi? Hawapendi sana kushinda nyumbani na familia.

Leo nina familia nimegundua kwamba kumbe ukipenda sana kushinda nyumbani mara nyingi utagundua vitu vingi ambavyo wakati haupo huwa vinachukuliwa kama vya kawaida lakini ukiwepo unaona kama ni upungufu.

Nafahamu sasa kwa nini wale wazee walikuwa hawapendi sana kushinda nyumbani kuepuka kuona udhaifu mwingi nyumbani badala yake wanaamua kushinda vijiweni kuepusha mengi.

Lakini kwa sababu naipenda familia yangu, nikasema siwezi kuwa nashinda vijiweni kwa sababu ku-kaa na familia mbali hasa watoto, naweza kujikuta napoteza upendo kwao na madhara yake hayatao-nekana sasa bali nikizeeka na kuhitaji malezi ya watoto, itakua hakuna mwenye mpango na mimi kwa sababu sikutengeneza mapenzi kwao wakiwa wadogo.

Kwa hiyo nafanyaje niwapo nyumbani? Jambo kubwa nalofanya ni kupuuza mambo mengi ninayoyaona ya yakitokea wakati nipo.

Najifanya kufumba macho na kuziba masikio huku nikiona na kusikia.

Njia hii mara nyingi inampa taabu sana aliyetenda jambo ambalo angetegemea kuambiwa kwa nini unafanya hivi, halafu haambiwi. Kwa vyovyote anaweza kupata hofu ya kutolitenda tena.

Nilipoanza shughuli za uandishi wa vitabu na makala mbalimbali sasa miaka mingi kidogo, nilipata ushauri mwingi ambao kwa asiye na roho ngumu, angechukulia kama ukosoaji na ukatishaji tamaa.

Ni kweli wakati mwingine inaumiza maana baadhi ya ushauri ulikuwa unakatisha tamaa.

Pamoja na kuupuuza nilijifunza kitu ndani yake.

Kilichonisaidia ni kukubali kwamba sikuwa najua kila kitu. Leo wale waliokuwa wakinikosoa ndio wanaonipongeza na ninawashukuru sana pengine wasingefanya hivyo leo nisingikuwa mwandishi mzuri kama wanavyosema wenyewe leo.

Wanaotakiwa kukosolewa ili waamue kupuuza au kutumia ukosoaji kwa ajili ya kujiimarisha, wanaposifiwa wakati wote hushindwa kuyatambua makosa katika utendaji wa kazi zao. Kumekuwa na wimbi kubwa la watu kuwasifu sana viongozi wetu.

Kusifu si jambo baya lakini sifa zinapozidi uhalisia huwafanya hao wanaosifiwa kushindwa kuona kasoro zao.

Njia bora ni kuwaacha ama wayapuuze au wayazingatie maoni yanayoitwa ya ukosoaji ili kujua wapi wanakosea.

Mara nyingi wanaojipa kazi ya kusifu wanazo ajenda zao na wanataka zifike mahali fulani na wakati mwingi matokeo ya juhudu hizo, matunda yake si ya umma bali ya binafsi.

Kwa hiyo kama tunaamua kupuuza tunaweza kupuuza sifa pamoja na ukosoaji.

Tukichagua kupuuza ukosoaji na kuzingatia sifa ni rahisi kuingia kwenye mashimo marefu ambayo hatutapata kamba ya kututoa humo.

Tusimlazimishe umbwa kwenda kula chakula kwa kumfunga kamba shingoni, badala yake tufunge kengele na tuigonge siku ya kwanza anapokuja anakuta chakula, hivyo kila wakati akiisikia ile kengele anajua ni chakula hata siku ikigongwa kwa bahati mbaya hakuna chakula atoke mate ya kutamani kula chakula.

Jambo fulani likizungumzwa likapuuzwa huwa mzungumzaji haendelei tena. Maana yake ukisifiwa ukaonyesha kupuuza hizo sifa, kesho hutasifiwa tena badala yake watakwambia ukweli.

Mara zote tukipenda kusikia mazuri tu kutoka kwa marafiki zetu wa karibu hatutapata kujua udhaifu wetu.

Badala yake tutapata habari za kufurahisha pekee ili tuwape vyeo wanaotufurahisha na ni vigumu sana kuendelea kimawazo kwasababu tunakua tumejifunga kwenye sifa.

Tunaweza kuamua kuzikubali sifa pamoja na ukosoaji au tukaamua kupuuza vyote lakini tukabaki kujifunza kutokana na mambo yote hayo mawili.

Anayesifu tujue kwa nini anasifu na anayekosoa tujue kwa nini anakosoa kwa sababu yote yana maana kwenye maisha.

Waliokuwa wakakinikosoa kwenye uandishi wangu, baadhi walikosoa na kunishauri namna bora ya kufanya.

Wengine waliishia kukosoa tu na sikuwahi kuwalaumu kwa sababu tayari wanakuwa wameshaonyesha eneo linalohitaji marekebisho. Si lazima washauri namna ya kufanya bali lilibaki kwangu ama kufanyia kazi au kuacha kama ilivyo na sikuwa na puuza yote.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Uzuri ni wa kuzaliwa nao, urembo umekuharibu sura*



Na Adam Fungamwango

**Utaona hapo binti wa Kiafrika anakuwa na nywele ndefu hadi mgongoni, na yeye anaanza kutingisha kichwa na kuziweka vizuri mara kwa mara akiiga wanavyofanya wa Kizungu, wao wakidhani ni mikogo au mbwembwe, kumbe wenzao wanafanya vile kutokana na usumbufu wa nywele hizo vichwani mwao.**

MWANAMKE ni kiumbe aliyeumbwa kwa ustadi wa aina yake na Mwenyezi Mungu. Wanawake wana uzuri wa asili ambao kila mmoja amejaliwa kuwa nao.

Si mbaya sana kwa mwanamke kujiongezea kidogo urembo kwa sababu ni asili yao. Mwanamke hawezi kutoka ndani kabla hajajitazama nguo aliyovaa kama imempendeza au la, ataangalia nywele zake, nyusi ili aongezee kidogo na wanja, atapaka 'lip stick' na kujiangalia sana kwenye kioo mpaka hapo atakapohakikisha kuwa yupo sawa.

Atafanya hivyo ili watu nje wamuone amependeza.

Na hili atalifanya hata kama aliyemwambia tutoke ni mumewe na hata iwe saa 1:00 usiku muda ambao watu hawawezi kuangalia vitu vingi vya urembo lakini hawezi kutoka hivi hivi tu. Hii ni asili ya mtoto wa kike.

Hata hivyo kuna vitu vingine ambavyo tumeletewa na wazungu vinavyokiuka mila na tamaduni za Kiafrika.

Kuna nywele bandia ambazo kazi yake ni kuwafanya baadhi ya wanawake kuona nywele za Kibantu walizonazo hazina maana yoyote zaidi ya zile za wazungu. Hakuna nywele bandia ambazo zinafanana na za mwanamke wa Kiafrika bali wa kizungu.

Nywele ndefu zinazofanana na za wanawake wa kizungu zenye rangi mbalimbali ndizo zinazouzwa madukani. Ili waonekane wamependeza na wa kisasa, baadhi ya mabinti wa Kiafrika wanajivika.

Kuna nywele za kupachika maarufu kama mawigi, halafu zingine ni za kushonea juu ya nywele nzuri za kibantu.

Utaona hapo binti wa Kiafrika anakuwa na nywele ndefu hadi mgongoni, na yeye anaanza kutingisha kichwa na kuziweka vizuri mara kwa mara akiiga wanavyofanya wa Kizungu, wao wakidhani ni mikogo au mbwembwe, kumbe wenzao wanafanya vile kutokana na usumbufu wa nywele hizo vichwani mwao.

Kama vile haitoshi, wanaleta na vipodozi vikali kwa ajili ya kuondoa ngozi asili na kuileta ile inayofanana na wazungu.

Wanawake wengi si Tanzania tu, bali Afrika nzima wameingia kwenye mtego huo. Baadhi yao ukiwaona unaweza ukadhani hawakuzaliwa kwenye bara hili.

Hapa nchini tunawaona baadhi ya wanawake wakijipamba kwa nywele hizo, kope bandia, nyusi zinavyonyolewa eneo halisi na wanja unapakwa juu yake kidogo na rangi ambao si ya asili waliokuwa nayo, ukijumlisha na 'make up', unaweza kumsahau.

Unaweza ukadhani siyo yule ambaye unamfahamu kile siku, labda mpaka yeye akuite.

Pia kama ndiyo siku hiyo mnafahamiana, halafu uko naye usiku mzima kesho aondoe wigi lake na 'make up' unaweza kabisa ukadhani umebadilishiwa mtu. Siyo yule ambao umekuwa naye usiku mzima.

Pamoja na yote hayo, mara nyingi vipodozi huwa na kemikali ambayo wakati mwingine inaharibu kabisa ngozi ya mtu au hata sura yake.

Hii imetokea sana kwa wanawake wengi, kiasi hata serikali kupiga marufuku baadhi ya vipodozi.

Ingawa wanawake wengi wa kizazi wamekuwa na tabia hii, lakini mwanamuziki Marijani Rajab alilio-na tangu miaka ya 1980, ambapo si tu hakukuwa na wengi wenye tabia hiyo, hata kuvipata vipodozi ilikuwa ni mbinde.

Vichache vilivyopatikana vilitoka Burundi, Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo) kupitia Kigoma na vilitumiwa na warembo wachache sana, watoto wa mjini, hasa waliokuwa wakiishi maeneo ya Kariakoo na Ilala tu.

Marijani alimwimba msichana Mayasa ambaye alitumia vipodozi vikali vikamharibu sura yake. Mwanamuziki huyo alielekeza kwa undani tukio lililomtokea mrembo huyo.

"Mayasa mbona wanichana mbavu bibie, sura yako mbona sasa imekuwa hivyo, nakuuliza mbona hata kunijibu hutaki, umenikasirikia kama mimi ndiye nilikutuma. Sura yako na ulivyokasirika mama ee, ndiyo mimi wazidi kunichana mbavu Mayasa oooh!

Dada yako jana alipita kunieleza, lakini mimi hata kidogo sikumuamini.

Kaniambia ulizidisha tamaa ya urembo, mawazo yako uwe mzuri kuliko ulivyoumbwa, Mayasa tizama sasa ulivyobadilika, urembo umekubadilisha sura yako hooo!

Nasikia ukachanganya madawa ya nywele, ukaona bado na mengine madawa ya ngozi, mchana kutwa hubanduki kwenye kioo, sijui mama ulitaka uwe sawa malaika, Mayasa tizama nywele zilivyoharibika, sura yako hapo zamani haikuwa hivyo hooo!

Oooh Mayasa, mama Mayasa, ooh Mayasa, uzuri ni wa kuzaliwa nao. Ooh Mayasa, mama Mayasa hoo, hapo zamani mama ulikuwa mwenye umbo la kupendeza.Ooh Mayasa, mama Mayasa haa, aliyekuona zamani akikuona sasa atashangaa.

Ooh Mayasa, mama Mayasa haa, tazama sasa dada, uzuri wako wa asili waupoteza. Ooh Mayasa, mama Mayasa haa, nakwambia kweli mama, aliyekuumba si mjinga."

Warembo mpo?

**Tuma meseji 0716 3505**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ONGEA na wifi yako anataka kukusalimu."

"Wifi yangu gani?"

"Kwani una wifi wangapi, bwana hebu msalimie." Alisema akiwa anamkabidhi Havijawa simu.

"Habari za huko wifi." Akasalimia kwa upendo na bashasha, salamu ambayo si tu ilimshtua, pia ilimtisha Sauda.

"Nzu...nzuri, nani wi...wifi." Akajibu kwa kigugumizi.

"Ndiyo mimi wifi yako, nakusalimia, nilikuwa na kaka yangu hapa tunaongea, akakupigia simu, nikamwambia na mimi nipe nimsamilie wifi yangu, nimemkumbuka, utarudi lini?"

"Kesho kutwa tunamaliza msiba, ukiisha tu narudi." Akajibu lakini akiwa na maswali mengi kichwani.

"Haya wifi yangu tutaongeza zaidi nikirudi." Akasema huku akimkabidhi kaka yake simu.

Dakika kumi baadaye, wakati Kassim akiwa ametoka nyumbani alisikia simu iliyokuwa mfukoni ikiita.

Akaingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake. namba ilionyesha ni mkewe.

Alijua swali atakaloulizwa. Ambacho hakujua ni kwamba litaulizwa kwa vipi.

"Enhee imekuwaje, huyo ni Havijawa kweli aliyekuwa akiongea au mwingine?"

"Ni yeye."

"Huyu huyu ninayemjua mimi?"

"Hakuna mwingine mke wangu."

"Kimemsibu kipi tena?" Akauliza tena. "Na wewe naye usitake kujua sana. Ni kwamba wifi yako amebalika na anataka ukija huku akuombe msamaha."

"Aniombe msamaha mimi?"

"Ndiyo wewe."

"He, makubwa! Unajua mnanitisha mimi, kuna nini huko kimetokea mpaka kabadilika ghafla tu. Au mna mipango yenu mtu na dada yake?"

"Hapana, ukija nitakuja kukupa mchapo nini kimembadilisha."

"Hebu nidokeze, wewe si mume wangu, utaninyimaje ubuyu?"

"Mke wangu, subira siku zote yavuta heri, hapa nilipo kuna watu kibao, wakisikia si vizuri. Ila kwa kifupi amebadilika.


Kilichombadisha nini. Ukija nitakwambia. Najua yeye hatokuambia, lakini mimi nitakupa hiyo habari. Na ukija sasa ujue unakuja kama kuanza ukurasa mpya wa maisha. Siyo yake tena."

"Enhee niambie imekuwaje, mbona sielewi huku nilikowaacha. Maana kama uchawi hivi siamini nilichokiona."

"Ndiyo uamini tena mke wangu."

"Maana nilivyopokewa na wifi yangu utafikiri ndiyo nimetoka kuolewa, tangu niingie kwenye nyumba hii sijawahi kupokewa au kusapotiwa kama hivi.

Na mabegi nimepokelewa. Kwani imekuaje? Umemuendea kwa mganga nini?" Sauda alishangaa na kutania kwa wakati mmoja.




**Kwamba Basi baba yenu alikichukua kiwanja hiki kimakosa, au kinguvu kutoka kwa mtu mwingine na kwa maana hiyo nyumba yenu ama muibomoe wenyewe au ibomolewe ili mwenye nyaraka halisi achukue eneo lake?"**

Mabadiliko aliyoyaona wakati anarejea kutoka kwao Kondoa yalimshangaza na kumtisha pia.

"Si uliongea naye kwenye simu wewe siku ile wakati uko kwenu? Alikwambiaje? Mumewe akauliza.

"Achoniambia ni kwamba atakuja kuongea nikirudi."

"Sasa umesharudi. Utashirikiana naye, hana neno tena, ila tumepanga kesho kutwa kutakuwa na kikao kwa ajili ya kukuomba msamaha."

"Kwa nini amebadilika ghafla hivi?"

"Tumemuweka kikao mimi na baadhi ya rafiki zangu, akakubali na kuomba msamaha."

Kassim hakutaka kumwambia tatizo la nyumba lililotokea. Akaona kwanza aende akashauriane na rafiki yake waliotengeneza mpango uliomfanya Havijawa kurekebishika.

Kesho yake alikwenda kwa rafiki yake Pembe ili kupata ushauri.

"Unataka kumwambia mkeo kuwa dada yako amebadilika kwa sababu mimi nilikuja nyumbani na kujifanya Ofisa kutoka Wizara ya Ardhi, nimekuja na kuwaambia nyaraka za ardhi ya nyumba yenu feki?

Kwamba Basi baba yenu alikichukua kiwanja hiki kimakosa, au kinguvu kutoka kwa mtu mwingine na kwa maana hiyo nyumba yenu ama muibomoe wenyewe au ibomolewe ili mwenye nyaraka halisi achukue eneo lake?"

"Ndiyo hivyo Pembe."

"Hapana Kassim, nadhani tutakuwa tunakosea.

Kwa ushauri wangu sitaki yoyote kati ya dada yako na mkeo ajue nini kimefanyika, ibaki siri kati yetu mimi na wewe.

Nia yetu wao wapatane na tumeshafanikiwa.

"Ukimwambia mkeo hili, kuna siku dada yako atakuja kugundua kuwa tulifanya mchezo wa kuigiza kwa ajili ya kuwapatanisha, anaweza kubadilika tena na kuwa mbaya kuliko mwanzo.

Fikiria siku ile nilivyojifanya Ofisa wa Ardhi alipolia na kukuomba msamaha kwa yote aliyoyafanya, leo aje kujua kuwa ilikuwa ni uongo na ilifanyika hivyo kwa sababu ya wifi yake. halafu hata mkeo ukimwambia kuwa wifi yake amebadilika kwa sababu ya jambo hili, ataona kumbe si kwamba amebadilika kutoka kwenye nafsi yake, ila kuna kitu kimembadilisha pamoja ni woga wa kubomolewa nyumba," Pembe alimfunda Kassim.

Akili yake ikakubaliana na kile alichoambiwa na rafiki yake Pembe. Akakumbuka jinsi dada yake alivyoangua kilio siku ile Pembe alipofika na kujifanya Ofisa wa Ardhi.

"Nadhani wewe ndiyo Kassim Kinate, sawa?"

"Ndiyo mimi!"

"Na wewe Havijawa Kinate, si ndiyo dada?"

"Ndiyo!"

"Mimi ni Ofisa kutoka Wizara ya Ardhi, nimekuja hapa kuwaambia kuwa nyaraka za adhi ya nyumba hii ni feki."

"Basi baba yenu alikichukua kiwanja hiki kimakosa, au kinguvu kutoka kwa mtu mwingine.

Naye mtu huyo ni marehemu, ila watoto wake walikuja ofisini na kulalamika kuhusu kiwanja hiki. Kuangalia eneo na namba kwenye nyaraka halisi tukaona ni kweli, ila kulikuwa na nyaraka nyingine.

Na tulipozikagua tukajidhihirisha kuwa ya marehemu baba yenu ilikuwa feki."

Akakumbukuka alipowaambia wabomoe wenyewe nyumba ili wenye hati halisi wachukue kiwanja chao la sivyo itakuja kubomolewa kwa amri wa mahakama, au kwa kuwasaidia mawazo ni kwamba watafute wakili ili aende kortini azuie ubomoaji kwanza ili utaratibu mwingine ufuatwe.

Akakumbuka jinsi dada yake alipomwambia atafute wakili, lakini yeye akakataa na kumwambia hawezi kufanya hivyo kwa kugharamikia nyumba ambayo mkewe anateseka, hivyo ni bora aondoke wakaishi kwingine mbali na hapo ili awe na amani.

Hilo lilimfanya Havijawa kuangua kilio na kuona sasa dunia imemuelemea kwani kama kaka yake ataondoka, yeye hana uwezo wa gharama za kuweka wakili ili kuzuia nyumba kuvunjwa na kufungua kesi. Akibaki peke yake nyumba itavunjwa tu. Hivyo akaona cha kufanya ni kumlilia kaka yake afanye kama walivyoambiwa na Ofisa Ardhi ili waendelee kuishi pale wakisubiri hatma yao.

Ili kaka yake akubali hilo ni lazima mkewe awe na amani na utulivu, aishi vizuri na mkewe na amuombe msamaha, kitu ambacho Havijawa alilazimika kukubali. Hilo ndilo lililombadilisha na si kingine.

Kassim na Pembe wakati wanafanya igizo hilo walijua kabisa mwisho wake utakuwa hivyo.

"Na hata siku ya kikao cha kuomba msamaha mimi naomba nisiwe mmoja watakaohudhuria."


"Kwa nini Pembe?"

"Kumbuka mimi nilikuja kwako na kujifanya Ofisa Ardhi, sidhani kama mtu wa aina hiyo anaweza kuhudhuria kikao cha ndugu, jamaa na marafiki. Itaanza kuzua maswali.

Mimi natakiwa kuja pale na kuwaambia kuwa mambo ya kesi yenu yanakwenda vizuri, ili waendelee kuwa na amani."

Kassim alimshangaa rafiki yake Pembe kwa ushauri, mbinu na mipango aliyoitumia ambayo imefanya siku mbili tatu tu zilizopita kushuhudia mkewe na dada yake wakipika, kuongea na kula pamoja.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# YUKO SALAMA

MWIGIZAJI mkongwe na mwenye wafuasi wengi katika mitandao ya kijamii, Wema Sepetu, amewata Watanzania kutokuwa na hofu na afya yake kwa sababu kwa sasa yuko vizuri.

Hivi karibuni kulienea uvumi kwamba Wema, alishambuliwa na mpenzi wake Whozu na kumsababishia maumivu makali.

"Mimi niko salama kabisa, nataka kuwajulisha niko sawa kabisa, naendelea kupona, niko sawa kabisa" amesema Wema Sepetu



# Single Sally ajivunia ujasiri

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Single Sally, ameendelea kujizolea umaarufu baada ya ngoma yake mpya 'Umenipa Ujasiri' kufanya vizuri.

Akizungumza na Nipashe, Single Sally, amesema moja ya sababu ya mashabiki kuupenda wimbo huo ni namna unavyowatia moyo vijana kuendelea kupambana kutafuta maisha.

"Nimefanya wimbo ambao umegusa maisha ya watu, hii ni heshima kubwa sana kwangu na unajua kwenye haya maisha bila uwepo wa Mungu ni ngumu kutoboa, ila wimbo huu Umenipa Ujasiri unakutia nguvu," amesema Single Sally.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUIMARAES ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imefanya mawasiliano kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26. (***AS***)

### MUSIALA AWANIWA LIVERPOOOL

LIVERPOOL ina nia ya kufanya dili la kiungo wa kati wa Ujerumani, Jamal Musiala, huku Bayern Munich wakiweka bei ya pauni milioni 100 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Football Insider***)

### MARMOUSH PIA AHUSISHWA

LIVERPOOL pia inahusishwa na uwezekano wa kumnunua fowadi wa Eintracht Frankfurt kutoka Misri, Omar Marmoush mwenye umri wa miaka 25. ***(Bild, via FourFourTwo)***

### ARSENAL YAMUWANIA DIAZ

ARSENAL inapanga kumnunua kiungo wa kati wa Real Madrid, Brahim Diaz na iko tayari kulipa hadi pauni milioni 60 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye hivi karibuni ameweka mustakabali wake wa kimataifa kuichezea Morocco. (***Football365***)

### SAVIO HUYO CITY

KLABU ya Manchester City imekubali kumsajili winga wa Brazil, Savio mwenye umri wa miaka 19, ambaye yuko kwa mkopo Girona ambayo ni klabu dada ya City, Troyes. (***Football Insider)***

### FERGUSON AGOMBEWA

KLABU za Brentford na Aston Villa zina nia ya kumsajili kiungo wa Bologna na Scotland, Lewis Ferguson mwenye umri wa miaka 24. (***TeamTalk***)

### ADARABIOYO MKATABA MPYA

KLABU ya Fulham inatayarisha ofa ya mkataba mpya kwa mlinzi wa England, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26. (***Mail***)

### HARRISON KUUZWA

LEEDS United iko tayari kusikiliza ofa kwa winga wa England, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 27, ambaye ametumikia msimu huu kwa mkopo kwenye klabu ya Everton. (***Football Insider***)

### KLOPP KUINOA UJERUMANI

KOCHA Jurgen Klopp bado anaweza kupata kibarua cha kuinoa timu ya taifa ya Ujerumani huku wakiwa tayari kufanya makubaliano kwa ajili ya kocha anayeondoka Liverpool. (***Football Transfers***)

### ADIDAS KUIKATA FEDHA MAN U

MANCHESTER United watapata adhabu ya kulipa pauli milioni 10 kila msimu wanaposhindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mujibu wa mkataba wao mpya wa jezi za pauni milioni 90 kwa mwaka na Adidas. (***Times)***

### MANE KUTUA WOLVES

KLABU ya Wolves inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Rochdale na England, Matheus Mane mwenye umri wa miaka 16 kwa ajili ya akademi yao. (***Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VITA YA MAN UTD, LIVERPOOL FA CUP

**LONDON,** England

United inasaka ushindi wake wa tatu mbele ya Majogoo hao huku wapinzani wao wakitaka....

KOMBE la FA limerejea wikendi hii kwa hatua ya robo fainali na leo Jumapili Manchester United atakuwa mwenyeji wa Liverpool katika uwanja wa Old Trafford, mchezo utakaopigwa kuanzia saa 12:30 kwa saa za Tanzania.

Mashetani Wekundu watakuwa wakitafuta kurudia ushindi wao wa tatu dhidi ya Liverpool kwenye shindano hilo la msimu wa 2020/21, lakini watakabiliana na Majogoo ambao wanawinda mataji manne msimu huu.

Wapinzani hao wamekutana mara moja tu kwenye Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu.

Mchezo wao wa mwisho ulimalizika kwa suluhu kwenye Uwanja wa Anfield, huku vijana wa Jurgen Klopp wakishindwa kupata ushindi dhidi ya timu ya Man Utd iliyokuwa haipo kwenye kiwango bora.

Mchezo huo utaamuliwa na mwamuzi, John Brooks huku rekodi za mechi tano zilizopita za Man United dhidi ya Liverpool ni ushindi mara moja na wakifungwa mara tatu na sare moja.

**Kuelekea mchezo huo, Man United inauwezekano wa kumtumia Rasmus Hojlund.**

Raia huyo wa Denmark alikuwa katika hali nzuri kabla ya kupata majeraha lakini yuko kwenye nafasi ya kuanza kesho pale Old Trafford.

Huwenda pia Man United ikawa na huduma za Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka baada ya kocha Erik ten Hag kuzungumza kuwa wapo kwenye hali nzuri kwa sasa.

Pia Mason Mount amerejea mazoezini, lakini Mashetani Wekundu hao hawatakuwa na Omari Forson, Anthony Martial, Luke Shaw, Tyrell Malacia na Lisandro Martinez.

Huku wao Liverpool wataingia kwenye mchezo huo wakiwa na nguvu nzuri na kiwango bora zaidi.

Katika mchezo huo wa leo, vikosi na mifumo yao vinaweza kuwa hivi

**Man Utd: Mfumo (4-2-3-1):**

**Onana, Dalot, Varane, Maguire, Lindelof; Mainoo, Casemiro; Garnacho, Fernandes, Rashford; Hojlund.**

**Liverpool: Mfumo (4-3-3):**

**Kelleher; Bradley, Konate, Van Dijk, Gomez; Mac Allister, Endo, Szoboszlai; Salah, Nunez, Diaz.**




# RASHFORD HAWEZI KUUZWA MSIMU HUU WA JOTO - TEN HAG

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesema Manchester United inakusudia kumbakisha Marcus Rashford msimu huu wa joto licha ya faida ya kifedha ambayo ingepata kwa kuuzwa kwa mshambuliaji huyo wa England.

Kuondoka kwa Rashford kungeongeza faida ya kifedha kwa United kwa sababu sheria zinazipendelea klabu kupokea ada kubwa ya uhamisho kwa wachezaji waliohitimu kwenye akademi zao.

Hilo limeifanya Chelsea kufikiria ofa za kumuuza Conor Gallagher licha ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kuwa mmoja wa wachezaji muhimu sana pale Stamford Bridge msimu huu.

Hali ya kifedha ya Man United imetajwa kuwa "imewabana" kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto, lakini Ten Hag alisema Rashford, ambaye alisaini mkataba mpya Julai, atabakia hapo Old Trafford.

"Hatukumpa mkataba mpya msimu uliopita wa miaka minne kwa nia ya kumuuza sasa," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari jana.


"Anapaswa kuwa sehemu ya mradi huu. Sio somo ambalo hatuzungumzii."

United itamenyana na Liverpool katika uwanja wa Old Trafford leo Jumapili wakitaka kukiondoa kikosi cha Jurgen Klopp kwenye Kombe la FA.

Ten Hag ana matumaini ya kuwa na Rasmus Højlund, Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka, wakati Mason Mount pia amerejea mazoezini baada ya kukosa miezi minne iliyopita kutokana na jeraha la mguu.

"Tulikuwa na wiki nzuri," Ten Hag alisema.

# Lewandowski hatamwogopa Mbappe




**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Robert Lewandowski, amesisitiza kuwa hamwogopi mchezaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, huku klabu hizo mbili zikiwa zimepangwa pamoja katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

PSG watakuwa wenyeji wa Barca katika mchezo wa mkondo wa kwanza kabla ya kwenda uwanja wa Olimpic Lluis Companys kwa mechi ya marudiano.

Mshindi wa mechi hii atakutana na kati ya Atletico Madrid au Borussia Dortmund katika nusu fainali, huku washindi wanne wa michuano hiyo, Arsenal, Bayern Munich, Manchester City na Real Madrid wakiwa upande mwingine wa droo.

Baada ya droo hiyo, Lewandowski alifanya mahojiano na Meczyki ambapo aliulizwa kuhusu matarajio ya kumkabili Mbappe kama mpinzani iwapo atajiunga na Real Madrid msimu ujao.

"Kucheza dhidi yake kwenye LaLiga itakuwa nzuri. Uhamisho huu ukitokea, sitaogopa na nitaiona vyema," alisema Lewandowski.

90 inaelewa kuwa Mbappe bado yuko katika mazungumzo na Madrid kuhusu kuondoka PSG msimu huu wa joto, na mkataba wake pale Parc des Princes utakamilika mwishoni mwa msimu.

Bado hawajafikia makubaliano lakini mfumo wa makubaliano upo.

Mechi ya mwisho ya Mbappe akiwa na PSG anaweza kucheza dhidi ya Madrid katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana na kwamba wako pande tofauti.

Lewandowski pia aliulizwa kuhusu mustakabali wake usio na uhakika ndani ya Barcelona, lakini alikaidi kwamba atasalia mahali hapo msimu huu wa joto.

"Hakuna maana kuendelea na hili. Kila kitu kiko wazi kwangu. Najua nitacheza wapi msimu ujao. Nitabakia Barcelona," aliongeza.

Lewandowski hajawa na kiwango bora sana msimu huu, akifunga mabao 12 pekee katika mechi 26 za LaLiga.

# Guardiola: Ni utamaduni City kupewa Real Madrid

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekiri kuwa anafurahia "utamaduni" mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa kuikutanisha timu yake na Real Madrid.

Baada ya miaka miwili mfululizo ya kukutana katika nusu fainali, City na Madrid zitapambana katika robo fainali ya mwaka huu.

Pande zote mbili zina ushindi mmoja kila mmoja, huku timu ya Guardiola kwa sasa ikishikilia sifa ya kujivunia baada ya kuitupa nje Madrid ikielekea kutwaa taji hilo.

"Inaonekana kama mila kidogo, miaka mitatu mfululizo kucheza na wafalme wa shindano," alisema Guardiola kuhusu droo hiyo.

"Natumaini tunaweza kuwasili katika wakati mzuri, lakini bado kuna wiki chache kabla ya mchezo wa kwanza kule Madrid.

"Watu wanaposema droo ni rahisi, unamdhoofisha mpinzani mwingine lakini sio lazima kusema Real Madrid ni nini kwenye mashindano haya. Unapocheza hatua za mwisho unacheza dhidi ya timu bora zaidi za Ulaya na hao ni Real Madrid.

"Lakini wapinzani wote ni wagumu sana, kila mtu anajua. Tulifurahi kabla ya droo kwa sababu ni fursa nzuri kila tunapokuwa hapa. Ni shindano maalum."

Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti alikiri droo hiyo haikuwa ya fadhili kwa timu yake, lakini akakiri ukweli kwamba timu yoyote inayotaka kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya italazimika kupitia Man City wakati fulani.

"Jiji ni moja, sote tunafikiria hivyo na itakuwa ngumu sana," alisema.

"Wazo tulilonalo ni kushinda shindano na ili kufanya hivyo, lazima ushinde walio bora zaidi.

"City inaweza kuwa bora zaidi Ulaya kwa sasa. Itakuwa ngumu, bila shaka, lakini ikiwa unataka kuwa mabingwa wa Ulaya," lazima uwaondoe.

"Itakuwa robo fainali nzuri na tutacheza nao kwa kujiamini, tukipambana hadi dakika ya mwisho kama kawaida. Sijui City wanafikiria nini huko, itakuwa sawa na hapa. Mwaka mmoja tulishinda, mwaka mmoja walishinda tutaona.

"Ni droo ya karibu sana. Karibu sana. Nadhani hakuna upendeleo."

## Simba yaingia 'chimbo'

INATOKA UK. 24

Mashujaa walikuwa na nidhamu, walirudi nyuma wote, kwetu sisi tulikosa mikimbio kule mbele ili kutengeneza nafasi, lakini kipindi cha pili alipoingia Onana na Saido (Ntibazonkiza) kusisimama kati namba tisa kulitusaidia kuwafungua, tukapata nafasi tukazitumia, kwa hiyo naweza kusema kuwa kipindi cha pili mikimbio yetu ilibadilika," alisema.

Matola pia alifurahi timu yake kutoka uwanjani bila kuruhusu bao na kumfanya kipa Ayoub Lakred kufikisha 'clean sheets' ya tano kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

"Leo tuna furaha hatujaruhusu bao tumetoka na 'clean sheet', kipa wetu Ayoub amefanya kazi kubwa sana pamoja na mabeki wake, tulikuwa tunaumiza sana kichwa kwa sababu mechi tatu mfululizo tunafungwa bao, inaonyesha kile tunachokifanya kwenye uwanja wa mazoezi kimeanza kufanya kazi," alisema kocha kiungo huyo wa zamani wa klabu hiyo.

Aidha mfungaji wa mabao yote ya juzi, Clatous Chama, akiwa sasa amefikisha jumla ya mabao sita, alisema kipindi cha kwanza hawakuwa watulivu mpaka pale kocha wao Abdelhak Benchikha alipowapa maelekezo nini cha kufanya kipindi cha pili.

Akizungumzia kipigo hicho cha juzi, Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohamed Abdallah 'Bares' alisema mabeki wake walifanya makosa ya kizembe dakika 17 za mwanzo wa kipindi cha pili yaliyobadilisha matokeo ya mchezo mzima.

"Ni makosa tuliyoyafanya tukiwa katika eneo letu la ulinzi, tumecheza na timu yenye wachezaji ambao wanaweza kuamua matokeo wakati wowote. Unapocheza na timu kubwa kama Simba wachezaji wako wanatakiwa kuwa makini wasiruhusu makosa ya kizembe na hicho ndicho tulichokifanya dakika 17 za mwanzo za kipindi cha pili tukaadhibiwa," alisema.

Matokeo hayo ya juzi yanaifanya Simba kufikisha pointi 45 na kupanda mpaka nafasi ya pili kwenye msimamo huku Mashujaa wakibaki katika nafasi ya 12 wakiwa na pointi zao 21.

# KIBABAGE KWENYE RADA ZA SIMBA SC

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba wakiendelea na maandalizi kuelekea kwenye mchezo wao wa robo fanali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, uongozi wa timu hiyo umeanza mikakati ya kuimarisha timu yao na macho yao yapo kwa nyota wa Singida FG anayeichezea Yanga kwa mkopo, Nickson Kibabage.

Imeelezwa viongozi wa Simba wameanza mazungumzo na wenzao wa Singida FG inayoongozwa na Rais wake, Japhet Makau, kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kumsajili nyota huyo.

Taarifa kutoka ndani ya uongozi wa Simba, zinaeleza kuwa wanamchukulia Kibabage kama mbadala sahihi na muda mrefu wa beki wao wa kushoto na nahodha msaidizi, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr'.

"Kwa misimu kadhaa tumeona hakuna mbadala wa Zimbwe na baada ya majadiliano ya uongozi na benchi la ufundi imemuona Kibabage ni sahihi, jina la Kibabage limekuja baada ya kuona mwenye uwezo wa kuwa mrithi wa Zimbwe Jr kwa wachezaji wazawa ni yeye,"

"Tayari tumepeleka ofa yetu na kuanza mazungumzo na Singida Fountain Gate FC na wakiridhia basi tunahitaji huduma ya beki huyo ambapo hata kocha Abdelhak Benchikha ameridhika kulingana na kiwango anachokionyesha," alisema mmoja wa vigogo wa timu hiyo.

Walipotafutwa vingozi wa Singida FG, kupitia Ofisa habari wao, Hussein Massanza alikiri kuwepo kwa mazungumzo baini yao na viongozi wa klabu ya Wekundu wa Msimbazi juu ya kuhitaji ofa ya Kibabage.

"Ni kweli mchezaji wetu Kibabage (Nickson ) kwa sasa yupo Yanga kwa mkopo hadi mwisho wa msimu , mkataba wake na timu yetu unatarajia kutamatika msimu ujao wa 2024/25.

"Tumepokea ofa kutoka baadhi ya timu ikiwemo Simba ambao wamewasiliana na uongozi wetu kwa lengo la kutaka saini ya nyota huyo baada ya kuonyesha kiwango bora siku za hivi karibuni," alisema Massanza.

hata hivyo alisema kuwa bado mapema sana kuzungumzia suala hilo kwa ndanio lakini jambo hilo lipo ingawa bado halifajikiwa muafaka.




Mkaguzi Kata Gambosi, Mkuu wa Polisi Jamii Wilaya ya Bariadi Insipekta, Francis Msuku (katikati), akicheza ngoma ya asili ya Kisukuma katika Uzinduzi wa Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Utalii lililofanyika Bariadi mkoani Simiyu jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Pamba FC yanusa Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Pamba FC yenye maskani yake jijini Mwanza imeonyesha dhamira yake ya kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya juzi kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya Mbeya City kwenye mechi ya Ligi ya Championship, iliyochezwa kwenye uwanja wa Nyamagana.

Pamba, ambao ni Mabingwa wa Jamhuri wa Muungano wa mwaka 1990, ilipata bao lake la kwanza dakika ya 17 likifungwa na winga wa zamani wa Simba, Haruna Chanongo ambaye pia alipachika bao la pili kwa mkwaju wa penalti dakika ya 48 huku bao la tatu likifungwa tena kwa mkwaju wa penalti dakika ya 71 na Salehe Feruzi.

Matokeo hayo yanaifanya Pamba FC kufikisha pointi 54 katika michezo 25 iliyocheza, ikisaliwa na mechi tano tu na ipo katika nafasi ya pili ya msimamo wa chini ya KanGold inayoongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 56.

Pamba ambayo kwa misimu mitatu mfululizo imekuwa ikijaribu bila mafanikio kupanda Ligi Kuu, ikikwama kwenye hatua za 'play off', msimu huu imeonekana kujidhatiti kupanda moja kwa moja ili kukwepa kwenda katika mechi za mchujo.

Kanuni ya Ligi cha Championship inasema, timu mbili zatakazomaliza nafasi za juu zitapanda moja kwa moja Ligi Kuu huku zinakazoshika nafasi za tatu na nne zitacheza mechi za mchujo na mshindi kwenda tena kucheza na timu itakayoshuka Ligi Kuu.

Kocha wa timu hiyo, Renatus Shija aliwapongeza wachezaji wake, lakini pia akawapongeza wapinzani wake kwa kuonyesha upinzani mkubwa licha ya kuondoka na ushindi huo mnono.

Pamba ilishuka daraja mwishoni mwa miaka ya 1990 na ilitamba sana ikiwa na wachezaji wengi bora kama Madata Lubigisa, Rajabu Msoma , Beya Simba, Nteze John, Kitwana Selemani, Fumo Felician, Paul Rwechungura, John Makelele, David Mwakalebela, George Masatu, Hussein Masha, George Gole, Khalfan Ngassa, Ali Bushiri, Mao Mkami, Alphonce Modesti, Juma Amiri Maftah, Hamza Mponda, Nico Bambaga na wengineo ambao wengi wao baadaye walinyakuliwa na klabu za Simba na Yanga.

## Ni mechi ya kisasi

INATOKA UK. 24

mechi yetu na Coastal Union, tulifanya makosa mengi, hata hivyo tumefanyia kazi makosa hayo na tupo tayari kwa mchezo huu wa kesho (leo), hatuna presha yoyote tumejiandaa vizuri," alisema Bruno.

Nyota wa Azam FC ambaye ameitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa kama ilivyo kwa Mzize wa Yanga, Yahya Zaydi alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kupambana kutafuta alama tatu muhimu dhidi ya Yanga.

"Hizi mechi kubwa kwetu tunazitaka na tumejiandaa , tunataka kulipa kisasi cha kufungwa kwenye mzunguko wa kwanza, tuna waheshimu wapinzani wetu tunafahamu ubora wao lakini pia nao wana mapungufu yao ambayo tutayatumia kupata matokeo mazuri," alisema Yahya.

# Michezo

Jumapili Machi 17, 2024

Nipashe


UKU. 22





## Rashford hawezi kuuzwa msimu huu-Hag





Feitoto

Aziz Ki

## Simba yaingia 'chimbo' kuiwinda Al Ahly CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuifunga Mashujaa FC mabao 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kwenye uwanja wa Azam Complex, kikosi cha Simba kinatarajiwa kuingia kambini leo kujiandaa na mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Simba itaanzia nyumbani Machi 29 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa kujaribu kusaka tiketi ya kucheza nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya vilabu Barani Afrika.

Akizungumza juzi mara baada ya mchezo wao dhidi ya Mashujaa, Matola alisema wakati kukiwa na mapumziko ya kupisha michezo ya kimataifa ya kalenda ya FIFA, wachezaji wakienda kwenye timu za taifa, kwao hakutakuwa na mapumziko, badala yake wataingia kambini kujiandaa na mchezo huo wa CAF.

"Kuna mapumziko, lakini sisi Simba hakuna mapumziko kwetu, tunakwenda kujiandaa na mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wachezaji wetu wanarudi majumbani, lakini kesho (leo), tutaanza rasmi kambi," alisema Matola.

Akizungumzia mchezo wa juzi dhidi ya Mashujaa, Matola alisema haukuwa mchezo mwepesi, iliwabidi kupambana hasa kipindi cha pili na kubadilisha mbinu za mchezo zilizowasaidia kupata mabao hayo mawili.

"Kipindi cha kwanza

INAENDELEA UK. 23

# NI MECHI YA KISASI, UBABE

## ●●● Yanga yataka kuendeleza ubabe ikitaka kujidhatiti kileleni, Azam yataka...

**Na Saada Akida**

Ni mechi ya kisasi na ya kibabe, ndivyo unavyoweza kusema kwenye mchezo wa leo ambapo Azam FC wataikaribisha Yanga kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa ukiwa mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika mchezo wa leo ambao Azam ni mwenyeji, anaingia kuumana na Yanga huku akiwa kwenye nafasi ya tatu baada ya kukusanya pointi 44 wakizidiwa kwa pointi nane na Yanga ambao ni vinara wa ligi hiyo.

Ikumbukwe kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza uliochezwa Oktoba 23 mwaka jana, Yanga waliibuka na ushindi wa mabao 3-2 huku kiungo wake, Stephan Aziz Ki akifunga 'Hat Trick'.

Mchezo wa leo ambao utaanza saa 20: 15 usiku, unakuwa wa 36 kukutana kwa timu hizo kwenye mashindano yote ambapo katika michezo hiyo Yanga wameshinda mara 17, Azam wameshinda mara tisa huku wakitoka sare mara 10.

Katika idadi hizo za mechi, Yanga wamecheza nyumbani mara 18 ikishinda mara nane na kutoa sare mara tano huku Azam FC wakicheza michezo 15 wakishinda michezo saba, wametoka sare michezo minne na kupoteza michezo minne.

**Vita ya Aziz Ki na Feitoto**

Yanga wanaingia uwanjani leo wakiwa juu ya msimamo huku pia nyota wake, Aziz Ki akiwa kinara wa upachikaji wa mabao akiwa na mabao 13 ikiwa ni bao moja tu zaidi ya kiungo wa Azam FC, Feisal Salum 'Feitoto' ambaye amepachika mabao 12.

Nyota hao wawili leo watakuwa na vita ya peke yao katika kufumania nyavu kwani kama Azi Ki atafanikiwa kufunga bao ataendelea kuongoza katika orodha ya wachezaji wenye mabao mengi.

Hata hivyo Feitoto naye ana nafasi ya kulingana na Aziz Ki au hata kumpiku kama atafanikiwa kufunga bao zaidi ya moja.

Kuelekea mchezo huo wa leo, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi alisema itakuwa mechi nzuri kwa kuangalia kwa sababu timu zote zinatumia staili moja ya uchezaji.

Alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu kila timu imejiandaa kupata matokeo mazuri, vijana wake wako tayari kwa sababu amewaandaa kiakili na kiufundi licha ya kutoka kucheza mechi mfululizo

"Ni ngumu sana kucheza mechi mfululizo, lakini tupo tayari kwa mchezo wa leo, licha ya kuwepo na majeruhi kwenye kikosi changu lakini nitajitahidi kupanga kikosi imara kitakachofanikiwa kupata matokeo chanya. Nafahamu Azam FC ni timu nzuri na inapokutana na Yanga wanakuwa wazuri zaidi lakini kikubwa tunaenda kutafuta pointi tatu muhimu," alisema Gamondi.

Aidha, alisema kwake hapati wakati mgumu kucheza mechi dhidi ya Azam FC, licha ya kuwa na taarifa kuwepo kwa mashushu wa Mamelodi Sundowns watakaoumana nao kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kwa sasa tunaangalia mechi iliyopo mbele yetu dhidi ya Azam FC, kila mchezo una mbinu yake, tutakavyocheza na Azam FC ni tofauti na tutakavyocheza na Mamelodi , kwa sasa akili zetu zipo kwenye mchezo na Azam, tunafahamu ina wachezaji wazuri, wanajua jinsi gani ya kufanya wanapokuwa na mpira , lakini nimewaeleza wachezaji wangu jinsi ya kucheza mchezo huo na niwaombe mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi uwanjani kuendelea kusapoti timu yao," alisema Gamondi.

Kwa upande wake, mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize alisema yeye na wachezaji wenzake wana hali nzuri na wanahamasishana kutafuta matokeo mazuri na kupambana katika mchezo wa leo.

"Tunafahamu ubora wa Azam FC, tunaenda kuyafuata yale yote aliyotuelekeza kocha wetu kupambana kutafuta matokeo, kama nitapata nafasi ya kucheza nitamuonyesha kuwa hajakosea kunipanga katika kikosi cha kwanza," alisema Mzize.

Pia alikiri kweli wachezaji wanafatiki kutokana na kucheza mechi mfululizo lakini kazi ya mchezaji ni kujituma na kutekeleza majukumu yake kwa weledi na watapambana kwa ajili ya timu.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry alisema maandalizi yao yameenda vizuri na wanafahamu ubora wa Yanga lakini hawaihofii.

Alisema wamesahihisha makosa ya mechi zilizopita na wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo ambao utakuwa wa ushindani mkubwa.

"Hatukuwa na matokeo mazuri katika

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >